Ishara Za Kimaandiko Za Wakati Huu

Tunawashukuru nyinyi kwa ajili ya hili. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, kwa ajili ya maombi.

Baba yetu wa Mbinguni mwenye rehema nyingi, tunakikaribia kiti Chako kikuu cha enzi na ukuu, usiku wa leo, katika Jina la Yesu Kristo. Tukijua jambo hili, ya kwamba tuna uhakika kwamba utatusikia. Hatuna jina lingine tunaloweza kuhakikishiwa ya kwamba utatusikia kwalo, bali Yeye alisema, "Kama mtaomba katika Jina Langu . . ." Kwa hiyo, tunaomba ya kwamba utatupokea katika Ufalme Wako, usiku wa leo.

Na jalia tuondoke hapa, tukisema, kama wale waliotoka Emau, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Baba, tunawazia juu yao kwenye hiyo asubuhi nzuri, ya kwanza, ya kupendeza ya ufufuo; Yesu akiwa hai na miongoni mwa watu; na hata hivyo wao (baadhi yao, waliompenda), hawakuutambua.

Ndivyo ilivyo usiku wa leo, Bwana, baada ya miaka elfu moja mia tisa: Wewe ungali hai na miongoni mwetu, na watu wengi hawatambui hilo. (Ingawa hao watu walipaswa kulifahamu, wanajua Maandiko yalisema Yeye angefufuka.) Lakini, Baba, nadhani ni wanadamu tu. Tusamehe, Bwana. Nasi tunaomba, sasa, ya kwamba neema yako itatutosha, usiku wa leo.

Pia jalia baraka Zako juu ya wale wote wanaongojea na wale walio chini ya matarajio kwa ajili ya uponyaji wa miili yao. Tujalie, Bwana, kwamba itakuwa, usiku wa leo, imani yao ipande juu na wakuamini. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

Kasisi Jack Moore, je! yumo humu jengoni? Kasisi Jack Moore? Unatakiwa kwenye duka la vitabu mara moja, Ndugu Jack Moore.

Tuna furaha kuwa hapa usiku wa leo, tena, katika utumishi wa Bwana. Na kwa matarajio makuu tukitumaini ya kwamba Mungu atakutana nasi juu ya msingi kwamba tunaninii . . . Ameahidi kukutana nasi.

Sasa, hatudai kuwa na nguvu zozote. Si—siamini ya kwamba tuna nguvu za kuwaponya wagonjwa. Hatuna nguvu, bali tuna mamlaka. Mnaona? Sio nguvu.

Tuseme, kwa mfano, ni—ni polisi amesimama huko barabarani. Ana uzito wa ratili mia moja na kumi. Na hapa

unakuja mlolongo mzima wa magari ukienda kasi kwa mwe—mwendo wa maili themanini kwa saa, injini za nguvu farasi mia tatu ndani yayo, nayo yanavuma barabarani, injini za nguvu farasi mia tatu. Mbona, maskini jamaa huyo hana nguvu za kulisimamisha moja la hayo, lakini hebu tu hiyo beji ing'ae kisha ainue mkono wake juu: hebu sikilizeni breki zikilia, angalieni yakiteleza upande mwingine. Sio nguvu zake zinazoyasimamisha, ni mamlaka yake.

Nalo Kanisa lina mamlaka kutoka kwa Yesu Kristo. "Katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; wakishika nyoka; ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hayo ni mamlaka Yake yaliyotolewa.

Sasa, vipi kama maskini polisi yuyo huyo anaogopa kuinua mkono wake na kuingia kwenye msafara huo wa magari? Afadhali avue nguo yake rasmi, airejeshe hiyo beji, kwa kuwa kamwe hatafaulu kama polisi.

Wala nasi kamwe hatutafaulu kama mwaminio, mradi tu tunaogopa kuyatumia mamlaka tuliyopewa na Yesu Kristo. Tunao ushindi. Haitupasi kuwa na ninii yoyote...haitupasi kupigania ushindi, tayari tunao ushindi. Yeye alitushindia, sio sisi; alitushindia. Sisi si Mshindi Mwenye Nguvu, Yeye Ndiye Mshindi Mwenye Nguvu.

Sasa kumbukeni, kesho usiku, Bwana akipenda, siku hizi kadhaa za kwanza usiku...

Ni aibu kabisa kuingia kwenye mji kama huu, na kufahamiana tu, kupeana mikono, kisha kuondoka. Na hilo—hilo si vema kwa watu. Si vema kwa huduma, hakika si vema, kwa maana huduma kidogo iko upande wa maajabu, nawe unakuwa na siku moja ama mbili usiku, kuninii, yapata siku mbili usiku, kuitambulisha, kisha kuanza kuwaombea wagonjwa. Nao watu wanakimbia kwenye mstari wa maombi, pasipo hata kujua kile kinachowaleta, kuurukia tu bila ufahamu. Inapaswa kuwekwa wazi na kuonyeshwa Kimaandiko, Neno kwa Neno, kwamba ni BWANA ASEMA HIVI. Na hiyo ni kweli. Ujumbe wa wakati huu kwa ajili ya Uzao mwaminifu wa Kifalme wa Ibrahimu kupitia Yesu Kristo.

Kwa kuwa sisi ni warithi pamoja na Ibrahimu, kulingana na ahadi. Kwa kuwa sisi ni wa Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja naye kwa ahadi, Uzao wa Kifalme; sio ule uzao kupitia kwa Isaka, huo ulikuwa ni wa kimwili, kupitia kujuana kimwili. Yesu alikuwa U—Uzao pasipo kujuana kimwili. Alikuwa...Alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Hatuokolewi kwa damu ya Kiyahudi, wala hatuokolewi kwa damu ya Mataifa. Yeye alikuwa si Myahudi wala Mmataifa. Alikuwa ni Mungu. Hakuwa, chochote pungufu ya Mungu. Mnaona? Alikuwa...

Tunajua Yeye alichukuliwa mimba kwenye tumbo la uzazi, biki- . . . la bikira, Mariamu. Mwanamke alikuwa tu ni kiangulia. Hakuwa . . . wala lile yai halikuwa lake, hilo halikuwa ni yai lake, wala haikuwa chembechembe hai ya mwanamume yeyote, wala chembechembe hai ya mwanamume; ambayo ni himoglobini, ambayo ni seli ya damu, imo ndani ya jinsia ya kiume; tunajua hilo. Kuku anaweza kutaga yai, bali kama hajakuwa pamoja na ndege wa kiume, halitaanguliwa kamwe. Anapaswa kuwa pamoja na ndege wa kiume, kwanza. Wa kiume hubeba se—seli ya damu, nao uhai umo katika damu.

Naye Huyu alikuwa ni Mungu, Mwenyewe, Ambaye, ninii . . . Sasa, Protestanti huamini ya kwamba lile yai lilikuwa ni la Mariamu. Yai haliwezi kupatikana bila mhemko. Kwa hiyo mnamfanya Mungu kufanya nini, basi? Mnaona? Mungu aliumba yai na seli ya Damu pia.

Yeye alikuwa ni Mungu, mwili wa Mungu. Tumemwona Mungu, tulimshika Mungu kwa mikono yetu. "Bila shaka siri ya uungu ni kuu: kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na malaika, akashikwa hapa ulimwenguni, akapokelewa juu Utukufuni." Kwa hiyo, tunaona katika jambo hili, sasa, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu aliyefanyika mwili. Yeye alifanya maskani pamoja nasi. Ali—alibadilisha hadhi Yake kuu kutoka kuwa Yule mkuu wa Milele, kama tulivyozungumza jana usiku, Yeye alikuwa ni sifa ya wazo Lake Mwenyewe. Alishuka huku chini, akafanyika Mwanadamu apate kumkomboa mwanadamu.

Mbona, ni hadithi ya kupendeza kuliko zote. Sioni jinsi watu wangeweza kubakia wenye dhambi na—na—na kujua hilo: jinsi ambavyo Mungu alifanyika mmoja wetu. Imeonyeshwa vizuri sana pale, jinsi ambavyo ningependa kuwahubiria hiyo, katika Ruthu na Naomi: Jinsi alivyofanyika M—Mkombozi wa Jamaa wa karibu, ilibidi awe Mkombozi, na ilibidi awe ni wa jamaa wa karibu. Na jinsi Mungu, katika Roho, asingeweza kuwa wa jamii yetu, ndipo akawa wa jamii yetu. Wakati Mungu alipomfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe, alikuwa ni mtu-roho, wala hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi. Ndipo, Yeye akamweka ndani ya udongo baada ya . . . katika hisi tano. Alimfanya mnyama aliye na Roho wa Mungu ndani yake. Sasa, sisi ni uhai wa wanyama. Tunajua hilo. Sisi ni mamalia. Mamalia, mnyama mwenye damu moto. Halafu basi, Mungu akashuka chini katika umbo la mwanadamu, kama mwanadamu alichukua mfano wa Mungu, ndipo Mungu akachukua mfano wa mwanadamu, apate kumkomboa mwanadamu, kumkomboa. Loo jamani, ni—ni picha ya kupendeza jinsi gani, jinsi . . . Ni jambo la ajabu jinsi gani tulilo nalo.

Sasa, usiku wa leo, ibada fupi tu. Niliwaweka muda mrefu jana usiku. Baada ya saa tatu, niliona watu walianza, mmoja anaamka, anatembea hapa, anatoka nje. Mbona, mnaona, hilo

linasumbua. Huondoa mawazo kutoka kwenye mkutano. Na inapofanya hivyo, sio kosa lenu, labda ilikubidi kuwahi basi ama chochote kile, nawe huna budi kuwa kule. Ninajua hilo linamaanisha nini. Nitajaribu kuharakisha.

Sasa, kesho usiku, Mungu akipenda, ninataka kuchukua fungu la kiinjilisti na kuwahubiria kesho usiku, Bwana akipenda.

Usiku wa leo, ninataka kusoma Maandiko fulani na kuwapa tu nukuu chache, kuweka tu msingi kidogo. Kwa sababu, kwa kuwa hamuuelewi Ujumbe huu, nanyi nyote, karibu kila mmoja wenu, ni wageni kwangu, na hamjui lolote juu ya Ujumbe, na kisha hamjui haya yote yanahusu nini, mnauendea tu bila mpangilio.

Ninawatakeni muelewe: Ni ahadi ya Mungu kwa ajili ya siku hii! Si—siku za Wesley zisingefaa kitu leo hii. Siku za Luther . . . Ilikuwaje kwa—kwa Walutheri? Wa Wesley walipata kuwa walikuwa wakiishi katika mng'ao wa nuru ya Kilutheri na ndipo Mungu akamwinua Wesley. Basi kuna shida gani—kulikuwa na shida gani na Wesley? Walikuwa wakiishi katika mng'ao wa Wesley wakati Pentekoste ilipoinuka. Sasa, kuna shida gani na Pentekoste? Wanaishi katika mng'ao wa Kipentekoste.

Mng'ao ni uakisi wa nuru, kama vile mazigazi barabarani. Ni mahali ambapo nuru imekuwako na ikaakisi nuru yake. Hilo lilikuwa ni jambo lile lile, kwamba walimkataa Yesu. Walikuwa wakiishi katika mng'ao wa nuru nyingine, ya nuru ya torati. Nao wamekataa, ama, walishindwa kumwona Masihi, wakati manabii wao wenyewe walisema kile hasa Yeye angefanya, jinsi angetambulishwa. Naye huyo hapo, sawasawa kabisa vile walivyosema angekuwa. Na hata hivyo wakashindwa kumwona kwa sababu walikuwa wakiishi katika mng'ao wa siku nyingine.

Nashangaa leo, enyi marafiki, "Hali yako ya sasa ingekutambulishaje na baadhi ya wale watu wa Biblia?" Sasa, wazia hilo. Hao Mafarisayo na Masadukayo wote na makundi makubwa ya kidini, na jinsi walivyokuwa wagumu na wakuu. Sasa, wazia tu. Ungechukua upande gani kama Yesu angalikuwa duniani? Sio hata, hakuna kanisa lingemkaribisha ndani, hakuna mtu, ila tu marafiki wachache. Sasa, mnajua hilo limetabiriwa tena katika siku za mwisho? Hiyo ni kweli.

Na hivi mlijua, pia, ya kwamba katika siku hiyo Yeye alidhaniwa kuwa ni mtu asiye na elimu, ni mwana haramu? Mlijua hilo? Mlijua alidhaniwa kuwa ni mtu aliyerukwa na akili? Siku moja, Yeye aliwaambia wanafunzi wake (aliangalia huku na huku, kulikuwako na wengi mno pamoja Naye), akasema, "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uhai ndani yenu."

Sasa, mnafikiri daktari ama mwanasayansi ama—ama mtu mwerevevu, mwenye akili angewazia nini? "Mtu huyo ni

mumiani na anajaribu kutufanya sisi sote kuwa mumiani. Ati tunywe damu ya mwanadamu? Tule . . .?"

Kamwe Yeye hakulielezea. Haikumbidi kulielezea. Uzao halisi, wa kweli, uliochaguliwa tangu zamani utalishika. (Ilidhihirishwa katika maskini yule mwanamke tuliyezungumza habari zake jana usiku; hata hivyo katika hali yake, alijua tu ilikuwa ni kitu gani, upesi.) Naye akasema (Kisha alikuwa na watu sabini ambao alikuwa amewaita, kuwa, "wanafunzi."), akasema, "Mtasema nini mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa juu mahali alikotoka?"

"Ati akipaa juu? Tumeona kitanda alimopembezewa. Tunamjua mama Yake. Tunajua hori alimozaliwa. Tunatoka kwenye mji huo. Yeye huvua samaki pamoja nasi, na kadhalika. Jamaa huyu ni nani? Mbona, sisi . . ." Vema, hilo lilikuwa ni gumu sana kwao kuamini, ndipo wakaondoka.

Kisha akawaambia wale kumi na wawili, "Nimewachagua ninyi kumi na wawili, na mmoja wenu ni ibilisi." Kisha akawaambia, "Mnataka kwenda, pia?" Sasa, Yeye kamwe hakulielezea. Kamwe hakuwaambia mwili Wake ulikuwa ni nini na Damu Yake ilikuwa ni nini. Kamwe hakuwaambia jinsi alivyoshuka chini na jinsi angerudi juu. Lakini angalieni, wakati wote, wala hao wanafunzi wasingeweza kulielezea, bali waliliamini. Wasingeweza kulielezea. Walichaguliwa kwa ajili ya huo Uzima. Wasingeweza kulielezea.

Petro akasema, "Bwana, twende kwa nani?" Waliujua Ujumbe wa wakati huo; walijua kile ulichopaswa kuwa. Wakasema, "'Tunajua ya kwamba Wewe, na Wewe pekee, unalo Neno la Uzima,' hakuna mahali pengine tunapoweza kwenda."

Ningeweza kwenda wapi, ni mahali gani leo, isipokuwa niende kwa Kristo, Biblia? Yeye ni—Yeye ni—Yeye ni Chemchemi ya Mungu isiyoweza kwisha; kadiri unavyoinywea, ndivyo inavyozidi kuwa jipya na bora.

Sasa, mkipenda, ninataka kusoma fungu dogo usiku wa leo, ama, kutusomea Maandiko fulani. Ndipo tutaenda moja kwa moja kwenye ujumbe (na kujaribu kutoka humu ifikapo saa tatu, ama baadaye kidogo, yote yakiwezekana), na hiyo itakuwa tu ni kama dakika thelathini, au thelathini na tano.

Naomba tusimame, tunapofungua Mathayo Mtakatifu 12. Mlango wa 12 wa Mathayo Mtakatifu, kuanzia kifungu cha 38, tunapoiinamisha mioyo yetu kwa kicho.

> *Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakisema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.*
>
> *Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; wala . . . hakitapata ishara* yoyote*, ila ya nabii Yona.*

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi; hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

. . .mtu *wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki,. . .watawahukumu kuwa wamekosea; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.*

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosea; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho *za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

. . .*tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

Na tuombe

2 Bwana, *tazama* maana yake ni "angalia, zingatia." Jalia tukumbuke usiku wa leo, Maneno haya, ya kwamba, "Hapa yupo aliye mkuu kuliko wote," Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Tunaomba baraka hii, ya kwamba atayachukua Maneno haya na kuyatia mafuta mioyoni mwa watu, kusudi wawe na imani, kisha ajionyeshe Mwenyewe yu hai kama alivyoahidi kuwa, "Lo, nipo pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari, ama ukomo." Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

3 Tutazungumza kwa muda mfupi tu juu ya: *Ishara Za Kimaandiko Za Wakati Huu.*

4 Sasa, Yesu hapa alikuwa akikikemea kizazi hicho kwa kuwa hawakuwa wameiamini ishara Yake ya Kimaandiko. Waangalie hawa Mafarisayo. Walimjia na kusema, "Mwalimu, twataka kuona ishara Kwako." Angalia upofu wao. Ishara ilikuwa tayari imefanywa nao hawakuitambua.

5 Je! mwajua, ninaamini ya kwamba siku moja Unyakuo utatukia na watu hawatajua lolote kuuhusu!

6 Yesu alisema, katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 11, wakati Yohana alipokuja kuninii. . .Ama, wanafunzi Wake walipokuja kumwona, kisha wakarudi. Naye akasema, "Mlitoka kwenda kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo, ama mtu aliyevikwa mavazi mororo? Ama mlitoka kwenda kumwona nabii?" Akasema, "Nawaambia ni nabii kweli! Sasa kama mnaweza kulipokea, mbona, huyo ndiye aliyenenwa habari zake na na—nabii, akisema, 'Mimi ninamtuma mjumbe wangu mbele ya uso Wangu.'"

7 Siku moja, wanafunzi walimwuliza, wakasema, wakati alipokuwa akinena habari za Yeye kuwa ndiye Mwana wa Adamu; alisema, "Ni kwa nini basi waandishi wanasema imempasa Eliya kuja kwanza?"

8 Sasa angalieni, katika Malaki mlango wa 3, ilisema ya kwamba, "Mimi nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu," Yesu alirejea kwenye Andiko hilo. Sio Malaki 4, sasa; huo ni wakati mwingine. Mnaona, Malaki 3 ilikuwa ni wakati mmoja, "Mimi ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu."

9 Malaki 4, atakapokuja, basi dunia itateketezwa, nao wenye haki watatembea juu ya majivu, katika ule Utawala wa Miaka Elfu, wala hatukufanya hilo baada ya kule kuja kwa Yohana. Bali itakuwa ni baada ya kuja kwa mjumbe wa siku za mwisho ambaye ataigeuza mioyo ya watu iirudie Injili ya asili, Imani ya baba wa mwanzoni, ya namna waliyokuwa nayo huko—katika Kanisa jipya huko Yerusalemu. Na hiyo itarejeshwa katika siku za mwisho, kwa . . . Litakuwa ni katika kundi la walio wachache sana, bali itakuwa na tabia ile ile kama ya Eliya na Yohana, wote wawili wapenda nyika, "wachukia wanawake," na kadhalika, na wakemea madhehebu. Na itakuwa tu ni mtu wa aina ile ile, bali atakuwa na ile Kweli, Kweli iliyothibitishwa, iliyotambulishwa. Imeahidiwa.

10 Sasa, tunajua ya kwamba Yesu aligeuka na kumwambia, "Eliya amekuja tayari, wala hamkumtambua."

11 Sasa hivi si ingekuwa ni huzuni sana, moja ya siku hizi, kama tukilipata kanisa huko kwenye wakati wa ile dhiki kuu? Sasa sipo hapa kuhubiri fundisho. Sifanyi hilo. Ninawaheshimu ndugu zangu. Lakini kama mtanisamehe, hebu niingize hili kwa muda kidogo tu. Mimi, kwangu mimi binafsi, hakika, ninaamini kanisa linapitia kwenye ule wakati wa dhiki, bali sio Bibi-arusi. A-ha. Bibi-arusi anaenda Nyumbani. Mnaona, Mungu anamtoa Bibi-arusi kutoka kwenye kanisa, kama vile alivyolitoa taifa kutoka katika taifa lingine, huko Misri. Mnaona? Bibi-arusi, hao ni masalio wa uzao wa yule mwanamke, Wateule. Hiyo ni kazi Yake kwamba ataweka mchoro wapi, lakini masalio ndiyo yanayokatwa kutoka kwenye huo mchoro. Uzao wa mwanamke ulikuwa huko katika giza la nje, kweli, bali sio—sio Kanisa teule. Hilo, Hilo tayari limehukumiwa na kusafishwa, kwa sababu liko ndani ya Kristo. Hailibidi kupitia kwenye kitu kingine chochote. Hao wengine hawana budi kupitia kwenye hukumu kwa sababu hawakuwa ndani.

12 Sasa, moja ya siku hizi, maskini hao wachache, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa kwa maji, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Katika siku za Lutu, ambapo nafsi tatu ziliokolewa kutoka kwa moto, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

13 Wanatazamia kitu fulani kikubwa mno cha ulimwenguni kote, wakati hata hakipo kwenye Maandiko. Mnaona? Moja ya siku hizi, wao watasema, "Vema, nilidhani Biblia ilisema ya

kwamba kanisa litayaepuka haya yote?" Bibi-arusi anayaepuka haya.

14 Na hebu wazia tu, baada ya Nuhu. . . "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Nuhu aliingia ndani ya safina nao mlango ukafungwa. Aliingia tarehe kumi na saba Mei, nao mlango ukafungwa, wala haikunyesha kwa muda wa siku saba baada ya yeye kuingia safinani. "Nao hawakujua." Mungu aliufunga mlango.

15 Na siku moja mlango wa rehema utafungwa. Nao watu wataendelea moja kwa moja wakidhani ya kwamba wanaokoka, na kuhubiri, na kadhalika, nayo rehema tayari imekataliwa kwa mara yake ya mwisho, wala hawajui mpaka itakapokosekana.

16 Kumbukeni, kuna mamia ya watu ambao hawajulikani waliko, kila siku, ambao hatuwezi kuwapata wala kutoa hesabu yao, kote ulimwenguni. "Mmoja atakuwa kondeni, nitamchukua mmoja, mmoja katika. . . Wawili kitandani, Nami nitamchukua mmoja." Kote duniani, kwa hiyo haitawachukua wengi sana katika kuondoka huko, Bibi-arusi aliyenyakuliwa. Kumbukeni ishara hizo.

17 Israeli daima walizitegemea ishara zao badala ya hotuba za kiakili. Walipaswa kufanya hivyo. Mungu aliwatumia manabii. Manabii wakawapa ishara.

18 Nazo ishara, daima wakati ikiwapo ishara, ishara ya Kimaandiko, inabidi pawe na sauti ya Kimaandiko itakayoifuata ishara hiyo ya Kimaandiko. Na yote haina budi kuwa ni ya Kimaandiko, iliyoahidiwa.

19 Kwa hiyo, mnaona, unaingia katika mtindo. Kama vile Luther katika kuhesabiwa haki, hilo ndilo yeye alijua; hivyo tu, waliridhika, nao wakaingia moja kwa moja katika fundisho lao. Huyu hapa Wesley akaja na utakaso, akaupita moja kwa moja; kisha akaunda dhehebu. Moja kwa moja ikaja Pentekoste pamoja na kurudishwa kwa karama; nao wakaunda dhehebu. Naye Mungu anasonga mbele moja kwa moja, mbele moja kwa moja, wakati wote, mnaona, kwa ajili ya kila siku, kila wakati wa Kanisa.

20 Mnayo picha ya kushangaza sana hapo, usiku wa leo, itakayoingizwa kwenye kitabu hicho, ya miaka mitatu, jinsi ambavyo Bwana amenijalia kuichora kwenye ubao, na kuonyesha tu jinsi zile Nyakati za Kanisa zingeshindwa, na kwamba ni lini na ni vipi zingeenda juu chini. Na mara huo ulipomalizika, yule Malaika mkuu wa Bwana, ile Nuru, mbele ya idadi ya watu kama wanaoketi hapa, alikuja moja kwa moja kando ya ukuta, akisimama pale. Nao watu wakizimia. Naye akaichora moja kwa moja, Mwenyewe, ukutani. Miaka mitatu baadaye, mwezi uliingia giza na ukapotea kabisa, kweli kabisa, kwenye ile siku. . . kabla tu papa, papa wa kwanza, kwenda Urumi.

21 Na wakati kanisa pamoja na baraza la ekumenia litakapokuwa tayari . . . Loo, ndugu, dada, msiniache nianze jambo hilo. Tupo papa hapa kwenye mwisho, kila ishara, kila kitu kimekaa vizuri kabisa.

22 Mungu hutoa ishara, ishara za Kimaandiko, ishara za Kimaandiko za sauti. Mnakumbuka wakati Musa . . . Je! ishara hutolewa kwa sababu gani? Ni kuvuta usikivu. Ishara ni ya kuvuta usikivu. Ndipo kama ishara hiyo haina sauti yoyote, basi ishara hiyo si sahihi. Na kama ishara inatoa maskini sauti ile ile ya kale ya kikanisa, ishara hiyo haitoki kwa Mungu, kama sauti hiyo haina badiliko. Na badiliko hilo halina budi kuwa ni ishara ya Kimaandiko, haina budi kuwa ni sauti ya Kimaandiko.

23 Tuseme, kwa mfano, sauti yake ya kimadhehebu iliifuata ishara fulani; Mungu kamwe hakuituma hiyo. Tumekuwa na madhehebu miaka hii yote. Haina budi kuwa ni kitu fulani tofauti. Haina budi kuwa ni BWANA ASEMA HIVI katika Maandiko. Mungu hana budi kuiahidi kwa Neno, ndipo ishara ni ya kuuvutia usikivu wa watu kwake. Ndipo basi sauti huifuata ishara hiyo, hiyo ni fundisho linaloambatana nayo.

24 Yesu alikuwa ni Mtu aliyewaziwa mema. Alikuwa ni rabi kijana, nabii wa Galilaya. Yeye, wakati alipokuwa akiwaponya wagonjwa, na kadhalika, Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri. Bali siku moja, Yeye aliketi chini, akaaanza kunena na kuwaambia, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja." Hiyo ilikuwa ndiyo sauti iliyoifuata. Loo, la, hawakutaka hilo. Walikuwa tayari kwa ishara, bali ile sauti hawakuitaka. "Mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa juu mahali alikotoka," wasingeweza kuliona hilo hata kidogo. Mnaona? Bali wakati sauti ilipoanza kuifuata ishara, hawakutaka uhusiano wowote na hiyo. Daima ni ishara na sauti!

25 Sababu ya Musa kuvua viatu vyake, ile ishara iliuvutia usikivu wake. Yeye aliangalia pale na akaona jambo hilo, mti huo ukiwaka moto.

26 Sasa, yeye alikuwa mwana kemia. Alikuwa mwanasayansi hodari. Alifunzwa katika hekima yote ya Wamisri. Nao walifanya mambo tusiyoweza kufanya leo hii, katika sayansi; kujenga piramidi, masfiniksi, walikuwa na mafuta ya kufanya mwili usioze ambayo hatuna, rangi ambazo hatuna. Ulikuwa ni ustaarabu mkuu kuliko, na wenye elimu nyingi zaidi, kuliko tulivyo siku hizi. Naye Musa alikuwa ndiye kiongozi wao. Basi alipouona huo mti ukiwaka moto, bila kuteketea, hapana shaka ila yeye alisema, jamani, moyoni mwake huenda alisema, "Nitaenda pale na kuchuma majani machache pale na kuyapeleka kwenye maabara, nione yamenyunyiziwa kemikali gani." Kama angalifanya hivyo, hiyo sauti kamwe isingalizungumza naye.

27 Huwezi kumwelewa Mungu. Inakupasa kuketi karibu Naye na kulizungumzia. Uvue viatu vyako, tuseme, uweke chini elimu yako. Uangalie moja kwa moja katika Neno Lake, na kusema, "Sijali yale mtu mwingine yeyote asemayo. Wewe umeliahidi hapa kwa ajili ya siku hii, na ni Kweli." Musa alivua viatu vyake.

28 Angalia sauti iliyotoka kwake. Kama isingalikuwa ni sauti ya Kimaandiko, Musa asingaliiamini. Hiyo ishara ilivutia usikivu, nayo ishara hiyo ilikuwa ni ya kuvutia usikivu wa nabii huyo.

29 Nabii, mwenyewe, ni ishara. Mungu anapomtuma nabii, kuwa macho, hukumu inafuata; daima imeifuata, daima itaifuata. Hakuna njia ya kukwepa. Na ina—inapita moja kwa moja juu ya vichwa vya watu, wala kamwe hawaijui mpaka imeenda mbali mno. Si ajabu Yesu alisema, "Mnajenga makaburi ya manabii, na kuyapaka chokaa, bali, nanyi ndio mliowaweka mle. Na kama walivyofanya baba zenu, nanyi mtafanya vivyo hivyo pia." Nao walifanya hivyo.

30 Sasa tunaona akija jukwaani sasa, tunamwona Musa akiinuka hapa. Naye alikiona kile kichaka, naye akakikaribia. Ndipo sauti ikatoka mle, ikasema, "Vua viatu vyako, maana mahali hapo unaposimama ni patakatifu." Akavua viatu vyake na kupiga magoti. Ndipo akasema, "Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo." Kukaja sauti ya Kimaandiko. "Nami naikumbuka ahadi Yangu, na ninayaona mateso ya watu Wangu. Naikumbuka ahadi Yangu, nami ninakutuma huko chini kufanya hivyo. Nami ninakufanya kama sauti Yangu.

31 "Nami nitakupa ishara mbili. Na moja ya hizo itakuwa mkononi mwako, nawe utamchukua na kumgeuza nyoka awe . . . ama fimbo iwe nyoka." Na—na jambo la pili, ni kuweka mkono wake kifuani mwake, na uponyaji wa Kiungu. Kasema, "Wasipoiamini sauti ya ishara ya kwanza, basi wataiamini sauti ya ishara ya pili. Na endapo hawaiamini, chota maji kutoka mtoni, uyamwage ardhini, nayo yatakuwa damu. Hiyo ni kusema, damu yao tayari imerowana ndani yake basi. Misri imekwisha."

32 Tumekuwa na ya kwanza, na tukapata ya pili. Sijui kama inayofuata si kurowana kwa damu. Nashangaa tunasimama wapi, usiku wa leo? Sauti na ishara, Mungu akiwapa ishara. La, wa—wazieni tu jinsi ambavyo mambo ambayo tumeona yakifanywa, Sauti za Kimaandiko, ufasiri.

33 Sasa katika mng'ao huu mkuu ambao watu wamekaa chini yake, macho yao yamepofushwa kwa huo mng'ao, "Mimi ni mshiriki wa *hili*. Mimi ni mshiriki wa *lile*." Hilo halina uhusiano wowote na Mungu kamwe, hata kidogo.

34 Mungu, katika kila kizazi amezituma ishara Zake. Yesu alisema, kabla ya Kuja Kwake Yeye angeonyesha ishara, kabla ya Kuja Kwake. Watu daima, kumbukeni, wanapaswa

kuamini ishara za Kimaandiko. Hazina budi kuwa ni ishara za Kimaandiko zilizotambulishwa. Mungu daima . . .

35 Kama nilivyosema jana usiku, kanisa huyachanganya mambo na kutoka nje, ndipo Yeye anamtia mafuta mtu mmoja. Kila mtu ni tofauti na mwingine. Yeye humtia mafuta mmoja. Mungu ni mmoja, na kwa hiyo Yeye humtia mafuta mtu mmoja. Kamwe Yeye hajawahi kulitumia kundi. Daima anamtumia mmoja; daima amefanya hivyo. Yeye kamwe habadilishi mwelekeo Wake. Humtumia mmoja. Naye humtuma huyo, anauhubiri Ujumbe. Unakataliwa, katakata; bali wote watakaokuja, watakuja, kutoka kwenye kizazi hicho. Zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, halafu ya saba, ndipo Bwana-arusi anakuja. Nasi tuko kwenye ya saba.

36 Nasi tunayaona makanisa haya ya kimadhehebu yakikimbia . . . Nami niliwaonea aibu hawa, ninyi Wafanya Biashara Wakristo, hivi majuzi usiku, mkiandika kwenye kile kitabu, kile kitabu cha Wafanya Biashara, "Baba Mtakatifu *Nanii*." Hivi ninyi Wapentekoste hamjui ya kwamba "hatupaswi kumwita mtu yeyote, 'Baba,' hapa duniani"? Hiyo inaonyesha ya kwamba namna fulani ya mng'ao imeyapofusha macho yenu. Naam. Na hivi hamtambui, hao watu, Biblia ilisema, wakati ma—wakati masalio haya "huyu bikira aliyelala alipokuja kununua Mafuta," ya kwamba hawakuyapata? Huenda walicheza katika Roho, wakanena kwa lugha. Bali nimewaona pepo wakifanya hivyo; hilo halina uhusiano wowote nalo. Ninazungumza juu ya Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu wa Biblia.

37 Nimewaona wakipiga makelele kwenye maeneo ya kipagani. Nimeizunguka dunia mara saba, katika ninii yote—katika kila namna ya wapagani, na karibu mamia ya maelfu, kadiri ya watu laki moja na nusu, naam, ama watu elfu hamsini wamekusanyika katika wakati mmoja. Na kuona jinsi ambavyo wachawi na kadhalika wanavyokupa changamoto kwake. Ni heri ujue kile unachonena habari zake. Ni vema usiwe na mazungumzo tu ya kiakili. Ni vema uweze, kwa njia ya Mungu, kuunga mkono kile unachonena habari zake, la sivyo usiende huko hudumani. Watakuaibisha.

38 Lakini, kumbuka, Mungu wetu angali ni Mungu wa Eliya. Angali ni Mungu aliyewahi kuwa. Angali ni Mungu yeye yule. Yeye hutenda kazi katika viwango vile vile. Anafanya jambo lile lile. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nimewaona wakisimama wameduwaa, wamepooza, na kuondolewa uwanjani. Mungu angali ni Mungu. Angalieni, sasa, Yesu alitwambia mambo haya yangetukia katika siku za mwisho, nasi tunaziona ni ishara za kuja kwake hasa. Kila kitu!

39 Sote tutakubali ya kwamba tuko katika mwisho wa dunia. Lakini wakati Yeye anapoanza kulishukia Kanisa, na mambo

atakayolifanyia Kanisa, ule Mwili, Bibi-arusi katika siku za mwisho, basi tunainua pua yetu juu na kuondoka. Mnaona, haina budi kuwa tu namna hiyo. Ulimwengu unainua pua yao kwa Hilo. Wanajaribu kulipuuza.

40 Angalieni vipindi hivi hapa vya televisheni, ambapo watu wengi mno wa Kipentekoste wanakaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia *Twampenda Sucy*, vitendo vichafu vya mwanamke fulani aliyeolewa mara nne ama tano, ama mwanamume fulani, nawe unakipenda hicho kuliko unavyolipenda Kani-. . .Kristo wako. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho, si ajabu tuna kitu kama hicho, wakati kuipenda dunia ni kubwa kuliko kumpenda Mungu aliye moyoni mwako.

41 Loo, tunaweza kwenda na kufanya uamuzi, na kuandika jina letu kwenye kitabu, na kutoka nje na kuishi pamoja na ulimwengu. Hivyo ndivyo ulimwengu unavyotaka. Hivyo ndivyo kanisa linavyotaka. Linataka kushikilia maungamo yake, na kuamini ya kwamba ni Mkristo, na kuishi vyovyote linavyotaka. Usijali, utafanya hilo kwenye baraza la ekumenia. Watakuruhusu kufanya lolote utakalo.

42 Lakini, kumbuka, Bibi-arusi atakuwa ameitwa, akatenganishwa na ni tofauti, akajazwa, akazaliwa kwa Roho Mtakatifu, akaoshwa na Damu ya Mwana-kondoo. Ataachana na kila kitu kilicho kichafu, karibu na Mume wake. Yeye ni bikira safi, mtakatifu, kwa Neno. Yeye na Neno ni kitu kile kile. Kama vile mtu na mkewe wanavyokuwa mmoja, katika ndoa, vivyo hivyo na Kanisa halisi la Mungu. Wakati anapokuwa ndani ya Kristo, Biblia inaitikiwa kwa "amina," kila ahadi. Haileti tofauti yoyote yale dhehebu lisemayo. Ile nafsi iliyo ndani ya mwaminio, huiitikia, kwa sababu ni Neno ndani yake likinena.

43 "Neno lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Biblia ilisema hivyo. Hivyo ndivyo inavyothibitishwa na kujulikana.

44 Angalia, ndugu yangu, angalia. Ni vibaya sana kwamba hatuyaoni mambo haya. Yesu alinena juu yake.

45 Yeye alikuwa ishara yao ya Kimaandiko, wala hawakumtambua. Alikuwa hasa ni ishara ya Kimaandiko. Aliwaambia alikuwa. Alisema, "Yachunguzeni Maandiko. Ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, msiamini."

46 Kila mtu ana fasiri yake binafsi. Kila dhehebu lina seminari hizi, zinazoangua kundi la wahubiri wa kiangulio. Daima nilimwonea huruma kifaranga wa kiangulio, hakuwa na mama; haidhuru atalia jinsi gani, hakulelewa na mama. Hivyo ndivyo mitambo hii inavyowatengeneza makasisi, wakati mwingine

hawamjui Mungu zaidi ya vile Mhotentoti anavyojua hekaya za Kimisri, ama sungura anavyojua jinsi ya kuvaa viatu vya theluji.

47 Tunachohitaji ni mhubiri aliye na ujuzi ambaye amekuwa upande wa nyuma wa jangwa, mpaka akakaa mahali hapo chini ya Mungu mpaka ile Nguzo ya Moto ikashuka mbele zake kama ilivyofanya kwa Musa, wala hakuna mtu anayeweza kumwondolea jambo hilo. Yeye alikuwapo pale wakati lilipotukia. Sasa hiyo ni kweli. Kumrudia Mungu, na kuirudia Biblia Yake!

48 Yesu alisema, "Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu."

49 Kila mtu ana fasiri yake mwenyewe. Methodisti wana yao. Mbaptisti, Mpresbiteri, Wapentekoste, hao wengine wote wana fasiri zao. Bali Biblia inasema, ya kwamba, "Neno la Mungu si la kufasiriwa apendavyo mtu binafsi."

50 Tafsiri Yake ni nini, basi? Yeye hujifasiria Mwenyewe. Alisema, "Iwe nuru," ikawa nuru. Hilo halihitaji kutafsiriwa. Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua. Hilo halihitaji tafsiri yoyote.

51 Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, Yeye angeimwaga Roho Yake juu ya wote wenye mwili," naye akaimwaga. Hilo halihitaji tafsiri yoyote. Tayari limefasiriwa, moja kwa moja mbele ya wakosoaji waliosema ya kwamba isingewezekana. Mungu alifanya jambo hilo, haidhuru, kwa maana Yeye analifasiri Neno Lake.

52 Yeye alisema hilo, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa mwisho, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa." Naye akafanya hivyo. Hakuna haja ya ufasiri wowote. Linajifasiri Lenyewe, ahadi hizi zote alizofanya Yeye.

53 Alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yale niyafanyayo, Yeye naye atazifanya." Halihitaji kufasiriwa, Yeye hulifanya tu. Hivyo tu. Kama . . . "Mimi Ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi." Uhai ule ule ulio kwenye Mzabibu umo kwenye matawi, tawi lile lile lililochipuka kwenye Siku ya Pentekoste.

54 Nilisimama hivi majuzi na kuona tamasha ya kiajabu. Rafiki yangu msiri, na rafiki ya Jack Moore. John Sharrit, Bwana alimbariki, sehemu ya kwanza ya huduma. Hakuwa na watoto. Alifanyia kazi senti ishirini na tano kwa saa, akibomoa saruji barabarani. Akaja mkutanoni, Bwana akambariki; akapata watoto watano, na sasa anamiliki nusu ya Phoenix. Yeye hutoa kadiri ya milioni mbili ama tatu, kila mwaka, kwa Bwana. Nilikuwa nimesimama shambani mwake, si muda mrefu uliopita, moja la hayo, ambako alikuwa amewaajiri kazi Wameksiko elfu moja mia tano. Na jimbo zima la pamba tupu, viazi, jimbo baada ya jimbo. Anayamiliki, yeye mwenyewe, na

miaka kumi na tano iliyopita alikuwa akipata robo kwa saa, kwa kubomoa saruji. Alimwamini Mungu.

55 Nilikuwa nikiangalia moja ya miti yake, nayo ilikuwa na aina nyingi mbalimbali za matunda juu yake. Yeye ana bustani kubwa za jamii ya mchungwa. Ndipo nikasema, "Ndugu Sharrit, vipi kuhusu ule mti pale?"

Akasema, "Ndugu Branham, huo una kila aina ya tunda."

56 Nikasema, "Vema, una malimau, una . . . Ninaona kangaja, chenza. Nimeona malimau, balungi, na machungwa." Nikasema, "Ni mti wa aina gani huo?"

Akasema, "Mchungwa."

Nikasema, "Ati mchungwa? Wenye hayo yote?"

Akasema, "Naam, hayo yamepandikizwa. Yamesukumizwa mle."

Ndipo nikasema, "Loo, kumbe. Huko ndiko mnakoita kupandikiza?"

57 Akasema, "Naam, Ndugu Branham." Akaelezea jinsi wanavyofanya, nyakati fulani za mwaka, jinsi walivyolipandikiza tawi hili.

58 Nikasema, "Sasa, mwaka ujao, hakutakuwako na kangaja zozote, hakutakuwako na machenza yoyote, hakutakuwako na tunda hata moja ila machungwa."

59 Akasema, "Loo, la. La, la." Kasema, "Mbalungi utazaa, tawi la mbalungi litazaa tawi la mbalungi, balungi. Mchenza utazaa chenza. Mlimau utazaa limau."

"Vema," nikasema, "huo ni mti wa aina gani?"

Akasema, "Mchungwa," akasema.

60 "Lakini kama mchungwa huo utazaa tawi lingine kamwe," nikasema, "litazaa kitu gani?"

Akasema, "Chungwa."

Nikasema, "Kumbe." Loo, naam. Kwa nini? Yote ni matunda jamii ya mchungwa.

61 Sote tunadai kuwa ndani ya Kristo. Bali wakati tunapoingia Mle ndani, pamoja na kanuni ya imani ya kimadhehebu, tunaishi Kwayo. Hiyo ni kweli. Bali kama Mti huo ukiwahi kuzaa tawi lingine, itakuwa ni Kitabu kingine cha Matendo kitakachoandikwa nyuma yake. Itakuwa kama tawi la kwanza lilivyokuwa, lililochipuza. Litakuwa limejazwa na Roho Mtakatifu, limevuviwa na Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu! Hakutakuwako na kanuni za imani kwake. Litakuwa ni Neno.

62 Wengi wenu mnaozichukua kanda zangu, mna Ujumbe juu ya *Mti Wa Bibi-arusi*. Tunda liko moja kwa moja juu yake, lipate ku—kuivishwa na Nuru za jioni. Sasa, nazo Nuru za jioni zinaliivisha hilo tunda wakati huu.

63 Sasa, tunaona walipaswa kumtambua, bali hawakumtambua. Ndivyo ilivyo katika wakati wetu, hawamtambui. Yesu hapa alikuwa akirejea... Upesi sasa, kusudi tuufikie Ujumbe. Yesu alikuwa akirejea nyuma, Naye alikuwa akifanya ishara, akiwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye yule Masihi, kile hasa Masihi alichopaswa kufanya, akifanya ishara ya Masihi. Loo, wengi wao, tulilichukua jana usiku, waliamini.

64 Tunaona ya kwamba yu—yule mwanamke kisimani, yeye hakuwa na elimu. Alikuwa na sifa mbaya. Bali mara alipoiona ile ishara, alisema, "Bwana, naona ya kuwa U nabii. Nami ninajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atafanya jambo hili."

Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

65 Ndipo alipoenda katika mji wa Sikari, na kuwaambia mambo yote aliyofanya, alisema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Haimkini kuwa Huyu Ndiye Masihi?" Nayo Biblia ilisema... Yeye hakulifanya jambo hilo tena, bali wao walimwamini, Yeye, kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke mwenye sifa mbaya. Sasa kunena kuhusu kusimama katika siku za Yona na kukihukumu kizazi hiki?

66 Angalieni, tunaona, basi, Nathanaeli, Petro, na wengine, walioamini. Tunamwona Batimayo kipofu.

67 Tunamwona maskini Zakayo juu mtini, amejificha. "Yesu," akasema, "Kamwe hataniona huku juu."

68 Ndipo Yesu akasimama moja kwa moja chini ya mti huo, akaangalia juu na kusema, "Zakayo, shuka chini." Yeye alikuwa ni Neno, Nalo Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni.

69 Nao Mafarisayo na wasomi wa siku hizo, walilihukumu, kwa sababu halikuwa na msasa na mng'ao wa kikanisa ndani yake. Halikuwa na msimamo wa kielimu linaopaswa kuwa nao. Halikuwa na mapambo ya kumetameta na—na kadhalika ambayo ukanisa unapaswa kuwa nayo, amevikwa kofia kubwa mno, ukosi uliopinduliwa, na kitu kama hicho, pamoja na namna fulani ya ma—ma—maneno angaliweza kuyanena, yasieleweke kabisa na watu wa kawaida.

70 Nayo Biblia ilisema, "Watu wa kawaida walimsikia kwa furaha." Yeye alizungumza lugha ya kawaida. Aliishi maisha ya mtu wa kawaida.

71 Ndipo tunaona ya kwamba katika kufanya jambo hili, tunaona kilichotukia. Sasa wasingeweza kuamini jambo hilo, ndipo wakasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ni pepo mchafu." Kwa maneno mengine, "Yeye ama anawasiliana kimawazo au—au ana ninii... Yeye, Yeye ni mpiga ramli wa namna fulani." Na mtu yeyote anajua ya kwamba huo ni wa ibilisi, na ni uigizaji. Na kwa hiyo tunaona ya kwamba basi wao walimhukumu.

Ndipo yeye alikuwa amesimama hapa, akasema, "Mwalimu, utuonyeshe ishara."

72 Yeye aliwageuzia nini? Alisema, "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara." Sasa angalieni, "Kizazi kiovu na cha zinaa." Alikuwa akitabiri. Akasema, "Nao wataipata, kizazi kiovu na cha zinaa." Na kama hicho si kizazi tunachoishi, sijui ni kwa nini. Kumbukeni, unabii wote una maana maradufu.

73 Nendeni pale kwenye Mathayo, mlango wa 3, mahali liliposema, "Kutoka Misri nimemwita Mwanangu." Angalia marejeo mpaka utakapoona Yeye alikuwa akizungumza juu ya Yakobo, Mwanawe. Bali pia Mwanawe mkuu zaidi, Yesu, Yeye alimwita kutoka Misri.

74 Sasa tunaona ya kwamba mle ndani, "Kizazi kiovu na cha zinaa chatafuta ishara, nacho kitaipata, kwa kuwa kizazi kiovu na cha zinaa kitaiona ile ishara ya ufufuo. Kama vile Yona alivyokuwa katika tu—tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi, kisha atafufuka." Imekuwa miaka elfu mbili, nasi tuna kizazi kingine kiovu na cha zinaa. Nao wanaipokea ishara ya Kristo aliyefufuka, akiwa hai miongoni mwetu, baada ya miaka elfu moja mia tisa! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

75 Yona, tunamjua, tunajua yeye alikuwa ni nabii. Wengi wao wanamtaja kama namna fulani ya m—mtoro. Hakuwa mtoro. "Wenye haki. . .hatua za wenye haki zinaongozwa na Bwana." Nilikuwa nikisoma kitabu fulani si muda mrefu uliopita. Yeye kweli alienda Tarshishi, ama alianza kwenda, badala ya Ninawi, bali hayo yote yalikuwa katika mpango wa Mungu. "Hatua za mwenye haki." Kwa sababu, wakati mwingine maovu yanakupata, ama kitu fulani.

76 Ndivyo ilivyokuwa kwa Ayubu. Yeye hakuwa. . .Ayubu alikuwa ndiye mtu mzuri kuliko wote nchini, katika siku zake, mtu mzuri kuliko wote ambaye Mungu angeweza kumpata, na hata hivyo angalia kilichompata. Yeye hakuwa akimrudi. Alikuwa akimjaribu. Alikuwa akimthibitishia Shetani Yeye alikuwa na mtu ambaye angemwamini hata katika matatizo.

77 Kwa hiyo Yona alikuwa ni kitu kile kile. Nasi tunamwona akienda zake Ninawi, naye akaingia meli ya kwenda Tarshishi, ndipo basi yeye. . . Nayo bahari ikainuka, naye alikuwa amelala. Akawaambia, "Nifungeni mikono na miguu, kisha mnitupe nje, kwa maana mimi ndimi nimesababisha jambo hili." Ndipo walipomtupa nje, nyangumi mkubwa alikuwa akiogelea hapo karibu majini, akiwinda, ndipo akammeza nabii huyu.

78 Ninakumbuka, si muda mrefu uliopita, huko Louisville, Kentucky, mahali nilipokuwa nikiishi ng'ambo ya mto huko Indiana. Walikuwa na nyangumi huko, kwenye be—behewa. Maskini Riki ambaye alikuwa na akili nyingi zaidi ya vile alivyojua kudhibiti, alisema, "Sasa mmesikia ile hadithi ya kale

ya uongo ya nyangumi kummeza Yona." Akachukua besiboli, akaiweka kwenye umio wa—wa nyangumi huyo, kisha akasema, "Angalieni hapa." Kasema, "Ni, besiboli hata haitaingia humo." Akasema, "Ile hadithi ya kale ya uongo ya—ya Yona akimezwa na nyangumi," akasema, "ni hadithi ya uongo tu." Hilo lilinizidia sana nisingevumilia.

79 Nikasema, "Hebu kidogo, bwana." Yeye akalielezea, akasema jinsi isivyowezekana kwa mtu kuingia kwenye koo hilo. Nikasema, "Unashindwa kuyasoma Maandiko, bwana. Wala hiyo si hadithi ya uongo. Ni ukweli."

Akaniangalia na kusema, "U nani wewe?"

Nikasema, "Mimi ni Kasisi Branham, kutoka tu ng'ambo ya mto huu."

Akasema, "Loo, kumbe, mhubiri anayeamini hilo."

Nikasema, "Kwa moyo wangu wote, kwa moyo wangu wote."

80 Ndipo akasema, "Vema, wajua," akasema, "angalia hapa, bwana, sio kubishana. Na ni—ninaupenda msimamo wako, na kadhalika, lakini," kasema, "kisayansi," kasema, "ni vigumu kuuingiza mkono wa mtu kwenye koo lake."

81 Nikasema, "Bwana, huyasomi Maandiko ipasavyo. Biblia ilisema huyu alikuwa ni samaki maalum 'aliyeandaliwa.' Hiyo ni kweli. Mungu alisema 'alimwandaa samaki.' Yeye ni maalum."

82 Ninaamini Mungu asemayo ni kweli. Huyo ni maalum. Akaitikisa pua yake juu chini, huku amevaa miwani, mara mbili ama tatu, kisha akaendelea na hotuba yake. Maal- . . . Ndipo kila mtu akacheka. Alikuwa ni samaki maalum. Mungu alimwandaa samaki apate kummeza Yona. Jamani! Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Sasa, tunaona, kwamba kwenye ninii yake . . . Yeye alimmeza.

83 Chochote, samaki, akiisha kula, hushuka moja kwa moja chini. Hebu mlishe samaki-dhahabu wako uone kilichotukia. Wanaingia moja kwa moja chini ya chombo ulimowaweka, na kupumzisha maskini mapezi yao chini. Maskini tumbo lao limeshiba, na kwa hiyo wako huko chini wakipumzika.

84 Kwa hiyo wakati samaki huyu mkubwa alipommeza Yona, hapana shaka alishuka chini, akapumzike, kutoka kwenye mawimbi na kutoka kwenye tufani. Yeye alikuwa akiangalia huko kupitia kwa uamsho, aone kile angeweza kupata; nao uamsho baharini, mwajua, ukivurumisha huku na huku, zile pepo. Kwa hiyo akampata mhubiri huyu na kummeza, kisha akashuka chini.

85 Sasa hapa, Yona huko chini katika tumbo la nyangumi huyu, huku amefungwa mikono na miguu yake, amelala kwenye matapiko ya nyangumi.

86 Sasa mara nyingi nimewasikia watu wakisema, “Niliombewa jana usiku, wala—wala mkono wangu haujapona. Ungali umelemaa. Ningali ninaumwa na tumbo. Macho yangu, bado sioni vizuri.” Loo, jamani! Kisha unamkemea Yona? Jamani!

87 Kama mtu yeyote alikuwa na kisa cha dalili, ilimbidi kuwa nacho. Kama aliangalia upande *huu*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi; upande *ule*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi, na mikono yake ilikuwa imefungiwa nyuma yake. Alikuwa katika tu—tumbo la nyangumi, chini ya bahari, labda kina cha mikono arobaini, chini ya bahari. Sasa nena kuhusu dalili! Halafu ukamwita aliyerudi nyuma.

88 Lakini mnajua alichosema? “Yote ni ubatili wa uongo. Hata sitayaangalia. Bali mara nyingine tena nitaangalia kwenye hekalu Lako takatifu, Bwana.”

89 Sasa, Yona alijua ya kwamba Sulemani alipoiweka wakfu hekalu, yeye aliomba na kusema, “Bwana, kama watu wako wakiwa katika shida mahali popote, nao waangalie mahali hapa patakatifu, basi wasikie kutoka Mbinguni.” Naye alikuwa na matumaini kama hayo katika maombi ya mtu aliyerudi nyuma, aliyefanya dua. Ni zaidi sana jinsi gani . . .

90 Hakuna mmoja wetu aliye katika hali hiyo, usiku wa leo. Hakuna mmoja wetu aliye na dalili kama hizo. Halafu tunaangalia dalili zetu? Kwa nini? Kwa nini? Kama angeweza kuwa na matumaini kama hayo katika maombi ya mtu aliyerudi nyuma . . . Nasi tunaombwa kuangalia Mbinguni, ambako Yesu ameketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, katika Hekalu isiyofanywa kwa mikono. Yeye anatarajiwa Mle ndani kufanya upatanisho unapokiri. Ni zaidi sana vipi sisi tungezipuuza dalili zetu, na, “Mara nyingine tena nitaangalia kwenye ahadi Yako takatifu, Bwana!” Loo, jamani, tunapomwona Mungu jukwaani!

91 Sasa tunaona ya kwamba, Yona, walisema nyangumi huyu alimbeba mle kwa siku tatu usiku na mchana, akamchukua kote akamrudisha, akairudia njia, akaenda. Na sasa watu wa Ninawi walikuwa, walikuwa wamekuwa kama walimwengu wengine sasa. Ulimwengu wao mkuu wa kibiashara, uchumi wao ulikuwa ni wa kuvua samaki, na wanaume wote walivua samaki. Nao waliabudu sanamu, naye nyangumi alikuwa ndiye mungu wa baharini. Basi siku moja, yapata saa tano, wakati hao wote walipokuwa huko nje wakivua samaki, huyu hapa mungu wao wa baharini anaingia, kisha akautoa ulimi wake, naye huyo nabii akatembea juu ya huo ubao wa kutokea. Si ajabu walitubu. A-ha. Mnaona? Hiyo hapo ishara. Hiyo ilikuwa ni ishara.

92 Sauti ilikuwa ni nini? Sauti ilikuwa ni nini, ati “Enyi wavulana mnaona ninaloweza kufanya?” La. “Tubuni, la sivyo

katika siku arobaini Mungu atapaangamiza mahali hapa." Ishara na sauti. Sauti iliyoifuata ile ishara, "Tubuni!"

93 Akasema, "Na hao watu wasiojua mkono wa kulia kutoka wa kushoto, walitubu kwa mahubiri ya Yona, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona." Mnaona? Ndipo akasema, "Malkia wa Kusini atasimama katika . . . kizazi chake . . . pamoja na kizazi hiki, na kukihukumu; kwa maana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani." Sasa wakati . . .

94 Katika kufunga, ninasema jambo hili. Wakati Mungu anapotuma karama duniani, karama ya ishara, nao watu wanaiamini, huo ni mmoja wa nyakati zenye fahari sana waliopata kuishi watu. Lakini anapoituma ishara nayo inakataliwa, kizazi hicho kinaingia katika machafuko. Imekuwa hivyo daima. Vipi kama watu wa Marekani, usiku wa leo, wangeipokea ishara ya Mungu katika siku hizi za mwisho?

95 Mbona, tunazungumza juu ya kwenda Fort Knox na kuihamisha serikali kule, na kuchimba chini ardhini. Mbona, makombora ya Urusi yanaingia labda yadi mia moja, mia mbili chini ardhini, na kuililipua urefu wa maili mia moja na hamsini, mbona, tetemeko hilo lingeingia moja kwa moja kwenye—kwenye lava. Hamko salama mahali popote juu ya dunia hii. Usalama pekee, huo uko mikononi mwa Yesu Kristo. Yeye Ndiye kimbilio letu.

96 Lakini vipi kama sisi, usiku wa leo, kama Wamarekani, nasi sote tulikitumainia kipawa ambacho Mungu alitupa, Roho Mtakatifu, katika siku za mwisho? Mbona, kila taifa lingetuogopa, kama walivyofanya katika siku za Sulemani.

97 Mungu alimpa Sulemani karama, na kanisa lote, kila mtu, aliiamini. Huo ulikuwa ni utawala wa fahari kwa Wayahudi. Huo ulikuwa ndio utawala wa miaka elfu wa Agano la Kale, katika siku za Sulemani, kivuli cha ule Utawala wa Miaka Elfu unaokuja. Wakati wa fahari kwa Wayahudi! Angalieni, hakuna mtu aliyeanzisha vita nao. Waliwaogopa, kwa sababu walijua Mungu wao alikuwa ni halisi. Kwa sababu, walikuwa Naye uweponi mwao, na watu wote walikuwa katika moyo mmoja na nia moja. Mbona, sifa ilisambaa kila mahali. Kila mahali, nanyi mnasikia, "Loo, ni jambo kubwa jinsi gani, Mungu mkuu Israeli waliye naye, Mungu aliye hai!"

98 Ndipo sifa zake zikafika Sheba. Hebu ipime kwenye ramani uone ni umbali gani. Kulikuwako na maskini malkia mmoja kule chini, aliyeanza kuona njaa moyoni mwake kwa ajili ya Mungu. Kila wakati angemsikia mtu fulani, mmoja wa ile misafara ulipopitia pale, angesema, "Je! mmepitia Palestina?"

"Naam."

"Hebu mniambie juu ya ule uamsho mkuu walio nao huko juu."

Na kila mtu angesema, “Loo, ni wa ajabu sana!”

“Je, mliuona?”

“Naam.”

“Ukoje?”

99 “Loo, yule Mungu mkuu wanayemtumikia ameshuka na anaishi ndani ya mmoja wa watumishi Wake, nao wakamfanya mfalme. Mbona, anaweza kutambua. Anajua mawazo hasa yaliyo moyoni mwako. Na, unajua, wanasema ya kwamba, ‘Mungu ni Neno, nalo Neno ni Mungu, nalo Neno linayatambua mawazo yaliyo moyoni mwao.’ Nayo hekima ya mtu huyo imepita chochote ulichowahi kusikia. Yeye anaweza kutambua na hata kujua mawazo unayowazia. Loo, ni uamsho wa ajabu walio nao huko juu.”

100 Nanyi mwajua, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu,” ahadi ya Mungu.

101 Ndipo maskini malkia huyu akaanza kuona njaa, naye alitaka kwenda kwenye uamsho huu. Sasa alikuwa na mambo mengi ya kukabiliana nayo. Sasa, jambo la kwanza, yeye alikuwa ni kafiri. Ingembidi kwenda kwa kuhani wake, kuomba kama angeweza kuondoka. Alikuwa malkia. Alikuwa mheshimiwa, mtu anayefahamika sana.

102 Sasa, hapana shaka alienda kwa kuhani mkuu, naye akasema, “Baba mtakatifu uliye mkuu, ninasikia ya kwamba kuna uamsho huko Israeli, nao wana wakati mzuri sana kule juu. Naye Mungu wao yu hai na anafanya ishara kuu na maajabu, ambayo hatujapata kuona kitu kama hicho, ama kusikia kitu kama hicho. Kila msafara, nimeulizia, nao wanasema ni ajabu sana. Je! naweza kuruhusiwa kutoka kwa dhehebu langu, niende nikatembelee?”

103 Ninaweza kuwazia, “Sisi hatushirikiani na mkutano huo, kwa hiyo afadhali usiukaribie.” Mnaona? Mwajua, mwanadamu hufa, bali sio roho. Mnaona? Ndipo tunaona, ya kwamba, “La, afadhali ukae mbali nao. Hatushirikiani na huo.”

“Vema, sasa, angalia, baba mtakatifu, ninasikia . . . ”

104 “Sasa angalia hapa! Kama kuna jambo lolote linaloendelea, lingekuwa likiendelea miongoni mwetu. Kanisa letu lingekuwa nalo.” Loo jamani! “Na ndilo hili hapa. Sisi, tungekuwa nao papa hapa.”

105 Ninaweza kumsikia maskini huyo malkia akisema, akisimama. Napenda ujasiri wake. Alisimama na kusema, “Nimeziona sanamu hizi zimesimama hapa kwa miaka mingi, nimekusikia ukisimama nyuma ya mimbara na kuhubiri juu ya mungu fulani aliyekuwako, mungu fulani aliyekuwako. Nyanya wa nyanya wa nyanya yangu aliisikia hadithi ile ile, wala haijapata kusogea wakati wowote. Wananiambia wana

Mungu aliye hai anayeishi miongoni mwao, kitu fulani ambacho ni halisi. Ninataka kukiona."

106 "Sasa, angalia! Kama ukienda, unajua vile utakavyofanya, unajihusisha na kundi la watu, wajua. Unajua, wana huku 'kufunguliwa kwa Bahari ya Shamu' na upuuzi huo wote wa namna hiyo. Afadhali usiende kule. Kwa sababu, ukienda . . . "

"Vema, ninaenda, kwa vyovyote vile."

"Tutalifutilia mbali jina lako moja kwa moja kutoka kwenye kitabu."

107 "Vema, liondoeni kwenye kitabu." Wakati mtu anapoanza kumwonea Mungu njaa na kiu, hakuna kitabu ulimwenguni kinachoweza kuwashikilia, kwa maana wanakitafuta Kitabu. "Liondoe jina langu mle ukitaka. Ninaenda, kwa vyovyote vile. Ninasikia ya kwamba huyo ni Mungu aliye hai, ana uhalisi. Ninaenda kutafuta kujua habari zake, kwa hiyo ni afadhali tu uliondoe jina langu kutoka humo."

108 Sasa alikuwa na mengi ya kumkabili. Sasa, kumbukeni, alijiamulia. Alichukua magombo yote, asome kile Yehova alichokuwa. Sasa, huyo hapo mwanamke mwerevu.

109 Usitegemee mawazo ya mtu mwingine. Shika tu yale Biblia isemayo ndivyo alivyo. Chukua yale anayosema kwamba ndivyo alivyo. Tafuta kujua jinsi Yeye alivyo, kama Yeye yu hai au la. Si yale msomi fulani amesema juu yake; bali yale Yeye aliyosema, Mwenyewe, kujihusu, kile alichoahidi.

110 Ndipo akaanza kusoma. Sasa, alikuwa na wazo zuri kwe—kweli. Akasema, "Nitabeba zawadi nyingi sana, nami nitazipeleka. Na kama ni kweli, nitauunga mkono. Kama si kweli, ninaweza kurudi na fedha zangu."

111 Yeye angeweza kuwafundisha Wapentekoste jambo fulani! Kuunga mkono vipindi vya redio ambavyo vinacheka kitu kile kile mnachoamini, na hata hivyo mnaviunga mkono. Hebu—hebu nini yenu . . . Vema, nitanyamazia hapo. Mnajua ya kutosha kulihusu, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kazi ya wahubiri wenu. Angalieni. Lakini hiyo ni aibu.

112 Akasema, "Kama si wa halisi, nitarudi na zawadi zangu." Kwa hiyo akazipakia juu ya ngamia. Kumbukeni, angalia yale yaliyomkabili. Alikuwa na safari ndefu. Mnajua inachukua muda gani? Ilimbidi kwenda kwa ngamia. Mnajua inachukua muda gani? Inachukua siku tisini. Miezi mitatu, juu ya mgongo wa ngamia, sio kwa kadilaki iliyoyoyozwa. La, la. Siku tatu, na juu ya mgongo wa ngamia.

113 Si ajabu Yesu alisema, "Atasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki, kukihukumu." Wapo watu, katika Birmingham, wasingevuka barabara kuona kitu kile kile. Mabasi, matramu, ndege, na kila kitu katika siku zetu! Si ajabu, watakapofufuka, watakihukumu kizazi hiki. Naam, bwana. Kwa maana, hapa

yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, Roho Mtakatifu Mwenyewe. Angalieni.

114 Tunaona, basi, kuna wazo lingine. Angalieni. Na sasa watoto wa Ishmaeli walikuwa jangwani, nao walikuwa ni maharamia, jamani, na wanyang'anyi. Mbona, alikuwa na fedha hizo zote mle! Kitu gani? Kundi lake dogo la matowashi, walinzi aliokuwa nao, na wajakazi wachache; wangewakatakata tu, vipandevipande, na kuichukua hazina hiyo na kutoweka kwa urahisi.

115 Lakini, mwajua, kuna kitu fulani kuhusu, wakati moyo wako unapoanza kuona njaa upate ukweli wa Mungu, hakuna hatari njiani. Huoni hatari yoyote. Huoni kushindwa kokote. Unasema, "Vema, je! nitapona?" Hakuna swali niani mwako. Imani halisi hujitia nanga yenyewe, hakuna kitu kitakachoitikisa. Inakaa papo hapo.

116 Kamwe hakuwazia juu ya hatari iliyokuwa mbele. Kuna kitu kimoja alichokuwa nacho, ku—kusudi moja alilokuwa nalo, jambo moja alilotaka kufanikisha. Na malengo yake yalikuwa ni sahihi, kwa hiyo akaenda akayatimize, kwa maana moyo wake ulikuwa ukiona njaa na kiu. "Heri ni wale wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa." Hiyo ni kweli.

117 Mwangalieni sasa anapoanza kulivuka jangwa, labda akisafiri usiku, akipumzika mchana chini ya oasisi, akiyasoma hayo Maandiko. Hatimaye, akawasili barazani mwa Sulemani. Alipowasili, katika—katika . . . Barazani, akapakua mizigo kwenye ngamia wake na kupiga hema.

118 Sasa, yeye hakuja kama baadhi ya watu, baadhi ya watu siku hizi. Yeye si ninii . . . Huu hapa mtindo wake wa 1964. "Nasikia wanafanya ninii . . . Wanasema Bwana anatenda haya. Nitashuka niende, na neno la kwanza litakalosemwa dhidi ya yale ninayoamini, mara moja nitatoka nje." Mnaona? Mnaona?

119 Bali si yeye. Yeye alilileta Neno na kuketi chini. Alikuwa atakaa hapo mpaka atakaposhawishika kweli. Hakuwa anaenda kuyachunguza mawazo yake mwenyewe. Alikuwa anaenda kulichunguza Neno.

120 Kwa hiyo akaingia. Nawazia, siku ya kwanza, aliketi chini, huko nyuma kabisa. Ndipo baragumu zikalia, kengele zikalia, na—na waimbaji wote wakaanza kuimba. Sanduku la Agano lilikuwa mahali pale. Ndipo Mchungaji Sulemani akatokea, akaketi chini. Yeye akasema, "Sasa nitaona kama Mungu yumo ndani ya mtu huyu ama la," kwa hiyo akaangalia. Ndipo kila kisa kikaanza kutokea. Loo, ni jambo la ajabu jinsi gani! Hakuna kilichofichika.

121 Kwa hiyo akapata kadi yake ya maombi, wajua, akangojea, kwa hiyo basi, yeye naye, akaanza kuja mstarini. Hatimaye, siku baada ya siku, akangojea. Wakati wote shauku yake ikaongezeka, wakati uamsho ukiendelea. Jamani, moyo wake

ulikuwa ukiona njaa! Baada ya kitambo kidogo, akafika mbele ya Sulemani, nayo Biblia ilisema, "Hakuna kitu ambacho Sulemani hakumfunulia," utambuzi!

122 Naye huyu hapa Yesu amesimama, Mungu wa Sulemani, "Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani." Mnaona?

Nao wakasema, "Utuonyeshe ishara, Bwana."

123 "Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Naye malkia wa Kusini alitoka pande za mwisho za dunia, ili asikie hekima ya Sulemani, na tazama hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani."

124 Nasi tumekuwa na elfu mbili, naam, miaka elfu mbili na mia nane, tangu wakati huo basi, wa historia ya Biblia. Na, usiku wa leo, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani, akiwa na Neno lililoahidiwa la siku hii, na bado tunasononeka hapo hapo. Si ajabu yeye atasimama katika ile Siku ya Hukumu na kuuhukumu Birmingham, Marekani, na mingine yote, kwa ushuhuda wake, kwa maana moyo wake ulikuwa na njaa ya kumwona Mungu naye akakaa mpaka ulipokwisha.

125 Alisema nini basi baada ya kuona jambo halisi likitukia? Unajua alisema nini? Yeye, baada ya Sulemani kumfunulia yaliyokuwa moyoni mwake, mbona, yeye alisema, "Yote niliyopata kusikia, na hata zaidi ya hayo." Kwa nini? Ilifanyika kwake wakati huo. Alikuwa ameona kile mtu mwingine alichosema juu yake, bali ilikuwa ni zamu yake wakati huo. Yake, alikuwa amefunuliwa siri yake. Naye akasema, "Ni kuu sana." Naye akasema, "Hata watu walio pamoja nawe wamebarikiwa, wanaoyaona haya wakati wote. Watu wanaosimama hapa na kuyaona mambo haya wakati wote, wamebarikiwa." Naye akaona jinsi alivyopanda kwenda katika nyumba ya Bwana. Akawa mwaminio.

126 Na imeahidiwa atasimama katika siku za mwisho na kuvihukumu vizazi hivi, kama ilivyokuwa katika siku za Sulemani, na kama siku za Yona, na kadhalika. Atasimama kwenye siku hii na kuhukumu, katika ule ufufuo, watu walioishi katika siku hii. Kwa maana, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Roho Mtakatifu Mwenyewe yupo hapa. Muumba wa mbingu na nchi yupo hapa, akijitambulisha Mwenyewe na watu Wake, akiwa na karama ya namna ile ile. Kama ilivyokuwa katika Kristo hasa; Yeye akifanya jambo hilo. Kama ilivyokuwa katika Sulemani; Yeye akilifanya. Kama ilivyokuwa katika manabii; Naye akilifanya. Kama ilivyotabiriwa kwa ajili ya siku za mwisho, hatujakuwa nayo kwa—kwa mamia na mamia ya miaka. Na kama ilivyokuwa kabla tu ya kuja Kwake mara ya kwanza, hawakuwa na—hawakuwa na utambuzi kwa mamia ya miaka, nayo hapo ikatokea jukwaani, na mtu fulani akamtambulisha Masihi. Na ikaahidiwa, jambo la pili litakalokuja moja kwa moja, katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa wakati huo.

127 Sisi hapa katika siku za mwisho: ishara alizoahidi kwamba zingetukia; hali ya ulimwengu jinsi hasa inavyopaswa kuwa; utovu wa uadilifu wa ulimwengu; na kila kitu tulicho nacho, mahali pake tu. Na Roho Mtakatifu moja kwa moja mahali pake, akifanya vile vile hasa. Loo, ni jambo zuri sana, kujua ya kwamba tunamtumikia Mungu aliye halisi.

128 Ninajisikia kusema jambo fulani sasa. Nimelisema hapo kabla, bali nafikiri. . . Ninajisikia kuongozwa kulisema tena. Kama vile kila mtu ajuavyo, mimi huwinda. Sana sana si kwa ajili ya wanyama pori; mimi napenda kuwa mwituni. Mama yangu alikuwa chotara. Mnajua jambo hilo. Mama yangu alikuwa nusu Mhindi wa Cherokee. Mama yake alipata malipo ya uzeeni, mnaona, hu—huko Tennessee. Kwa hiyo sasa tunaona ya kwamba, katika hilo, napenda kuwinda. Wala wongofu wangu haukuondoa jambo hilo, maana mimi . . .

129 Biblia yangu ya kwanza ilikuwa ni mwitu. Ningeweza kuona ua, jinsi lilivyokufa. Maskini ile mbegu ndogo ilikaa ardhini na kuoza, kila kitu kilikuwa kimekwisha. Lakini, mwaka ujao, usingeweza kupata chochote. Ungeweza kupeleka konzi hilo la mavumbi kwenye maabara, hakuna mwanakemia ulimwenguni angeweza kuipata chembechembe hiyo ya uhai mle ndani. Bali iliishi tena wakati jua lilipochomoza. Iliishi tena, na hiyo ilinijalia kujua kulikuwako na uhai, mauti, kuzikwa, kufufuka.

130 Ninaona jua likichomoza, asubuhi, ni mtoto mchanga aliyezaliwa. Kwenye saa mbili, linaanza kwenda shuleni. Ni kama saa nne, limetoka chuoni basi. Halafu saa sita, lina nguvu nyingi. Saa nane, lina umri wa miaka hamsini na mitano. Ndipo yapata saa kumi, linafikia kwenye themanini, themanini na mitano, limekwisha. Limetumikia kusudi la Mungu. Lakini nini? Kama lilitumikia kusudi la Mungu, je! huo ndio mwisho wake? La. Linachomoza tena kesho yake asubuhi, kushuhudia kuna kuzaliwa, uhai, mauti, kufufuka.

131 Lakini, jambo la kwanza, mbe—mbegu inapopandwa ardhini, kama haijarutubishwa, haitachipuka. Haina budi kulitumikia kusudi la Mungu, kusudi ipate kuchipuka. Nasi pia. Sisi ni mbegu iliyorutubishwa, ardhini, nasi hatuna budi kulitumikia kusudi la Mungu la sivyo kamwe ha—hatutafufuka katika ule ufufuo wa kwanza; tutakuja hukumuni katika ule wa mwisho. Ni kama tu mahindi chotara, yanachipuka muda mrefu kutosha kuistahimili hukumu yake ya jua, kisha inakufa na kurudi, wala hakuna lingine kwake. Kweli kabisa. Bali mbegu halisi inaondoka kwenye . . . huishi tena, inajizaa yenyewe.

132 Angalia utomvu kwenye mti. Kabla ya jalidi yoyote kushuka, ama chochote kile, mti huo ninii. . . Maumbile fulani, mahali fulani, huushika, yanasema, "Shuka upesi uingie chini ya huo mti, upesi sana. Shuka ukaingie ardhini, maana jalidi yaja." Na kama hauingii, utaua huo mti. Nao unajificha kule chini mpaka

mgando wote umekwisha, ndipo unapanda juu tena. Akili fulani hutekeleza jambo hilo. Unajua Akili hiyo ni nini? Hebu nielezee jambo hilo, ni akili gani inayoufanya mti huo kushuka chini, unajificha halafu unarudi tena, nami nitakwambia ni Akili gani inayoniambia kwamba wewe ni nani na unakotoka, yale umefanya na mahali uendako. Na hicho ni kitu kile kile, maana ni Mungu yeye yule. Hakika. Kweli kabisa. Mungu ndiye anayefanya mambo hayo. Sasa, kumbukeni, enyi marafiki.

133 Siku moja nilikuwa nikiwinda mahali nilipokuwa nimezoea kwenda kuwinda, huko kwenye misitu ya kaskazini. Nami niliwinda pamoja na rafiki mmoja, nami nilipenda kuwinda pamoja naye. Yeye alikuwa ni Mhindi nusu, pia. Naye. . . hiyo, Bert Call, naye ni mtu mzuri. Huenda mtu huyo ameketi papa hapa sasa, nijuavyo mimi. Yeye huja huku kusini wakati wote. Naye alikuwa ni mwindaji hodari. Haikubidi kuwa na wasiwasi juu yake. Hatapotea. Tunawinda pamoja nasi tunafahamiana, bali alikuwa ni mtu katili kuliko wote niliopata kukutana nao maishani mwangu. Angewaua watoto wa paa, kuninii tu—kunifanya tu nijisikie vibaya, maana sikupenda kukuona ukiwaua maskini jamaa hao.

134 Ni sawa kumuua mtoto wa paa, sasa, kama serikali ikisema hivyo. Nilikuwa bwana nyama, kwa miaka kadhaa, na ningali ni mhifadhi. Ni—ninaamini katika wanyama, nami ninaamini katika kuhifadhi. Na hebu wa—waninii tu. . . Ukiwaacha waendelee, watakaa hapa kula. Usipowala wengine wao, basi watashikwa na ugonjwa na kufa, ama wafe kwa njaa. Lakini ni yale tu sheria isemayo, wao wanajua jinsi ya kushughulikia jambo hilo. Acheni walishughulikie.

135 Lakini Bert angewaua apate tu kuwa katili, apate kunifanya nisikie vibaya. Yeye alizoea kusema, alisema, "Billy, wewe ni mhubiri mzuri, ama mwi—mwindaji mzuri, lakini, shida yako ni kwamba, wewe ni mhubiri kupindukia. Wewe ni mwoga kama kuku."

136 Nami nikasema, "Bert, wewe ni katili tu, hakuna lingine." Nasi tungeendelea.

137 Siku moja, nilipanda kule, ilinibidi kufanya kazi mpaka nikachelewa, na ilikuwa kidogo msimu umeenda sana. Ndipo yule kulungu mwenye mkia mweupe, sijui kama mnao hapa ama hamna. Loo, jamani, nena kuhusu Houdini kuwa mwanasanaa mtoro, hao ni bora kuliko yeye. Kwa hiyo majira yalikuwa yameenda; walikuwa wametupiwa risasi mara chache. Nasi tulianza asubuhi moja, yapata inchi sita za barafu, tukaanza kupanda kupitia kwenye Safu ya Milima ya Kirais.

138 Nasi tukachukua baadhi ya ninii, daima tulibeba chokoleti moto na sandiwichi. Na yapata adhuhuri, kama hatukumpata kulungu, basi tungetengana milimani, kisha turudi; tuingie, wakati mwingine, saa tatu ama saa nne usiku huo. Kama

tulipata kulungu, tulimtundika juu. Tulijua mahali tulipokuwa, nasi tungerudi na kumpata.

139 Kwa hiyo asubuhi hiyo tulipanda juu, na kwa hiyo, kabla sijaondoka, yeye alisema, "Aisee, Billy, nina kitu fulani kwa ajili yako mwaka huu."

Nami nikasema, "Ni kitu gani?"

140 Akaingiza mkono ndani ya mfuko wake na kutoa filimbi ndogo, kitu chenye ukubwa kama *huu*. Ndipo akaipiga, nayo ilisikika kama mtoto wa kulungu akimwita mamaye; mwajua, maskini mtoto mchanga wa kulungu akimwita mamaye.

141 Nikasema, "Bert, usingekuwa katili namna hiyo, sivyo?"

142 Akasema, "Loo, enyi wahubiri waoga kama kuku, nyote mnafanana."

143 Kwa hiyo tukaanza kupanda kilima, na yapata saa tano, yeye . . . Kulikuwako na mwanya yapata ukubwa wa chumba hiki, labda mkubwa zaidi. Wala hata hatukuwa tumeona alama za nyayo za wanyama. Ilikuwa ni wakati wa mbalamwezi, nao walikuwa wakila usiku. Nao walikuwa tu . . . Na ni vigumu kuwapata. Walikaa tu mafichoni, wamelala, na hivyo chini ya vichaka na huko nyuma kwenye msitu mkubwa. Nao wangeparura chini na kula majani aina ya moss, na kusahau. Kwa hiyo basi tungeninii . . .

144 Nikafika kwenye mwanya huu mdogo pale, naye akaketi chini. Nilifikiri alikuwa . . . lundo la barafu pale, mkondo. Nami nilifikiri alikuwa akiingiza mkono mfukoni mwake, namna *hii*, kutoa chupa yake ya themosi na kunywa chokoleti ya—yake, nasi tule chakula che—chetu cha kutwa kisha tutengane, ndipo tungerudi nyuma kuzivuka hizo safu; aende njia moja, nami nyingine. Lakini wakati alipofanya hivyo, nilianza kuunyosha mkono nitoe sandwichi yangu, maana nilikuwa kidogo ninaanza kuhisi njaa. Ndipo nikaiweka bunduki yangu chini kuegemea mtini, na kuingiza mkono kwenye mkoba wangu, ndipo nikamwangalia. Akaniangalia. Naye alikuwa na macho kama tu ya mjusi, hata hivyo, mwajua; kama vile wanawake wanavyoyapaka rangi macho yao, leo hii, mwajua, huo mtazamo wa kuchekesha kama wa mbwa juu yao, halafu yalikuwa yote yamepakwa rangi namna hiyo. Vema, hivyo ndivyo macho yake yalivyoonekana, kama ya mjusi, kidogo yameelekea upande. Akaniangalia. Nikawazia, "Ana mawazo gani?" Akaingiza mkono na kutoa filimbi hii ndogo. Nami nikawazia . . .

Nikasema, "Bert, hivi huna aibu?"

145 Naye akaipiga, na, alipofanya hivyo, yapata tu yadi thelathini, ama si hata umbali huo, kulungu mkubwa wa kike akasimama. Sasa, kulungu wa kike ni kulungu mama. Huyo alikuwa ni mtoto wake akiita. Yeye . . . Akapiga hiyo filimbi. Kulungu akasimama mara moja. Sasa yeye asingefanya

hivyo, kwa vyovyote vile. Alijua tulikuwa pale. Ila mtoto wake mchanga alikuwa hatarini. Naye akaniangalia, hayo macho ya mjusi tena. Nikamwona akiishusha kinga, juu ya bunduki ya thelathini-sufuri-sita. Yeye alikuwa hodari wa shabaha. Loo, alikuwa ni hodari.

146 Ndipo akaipiga ile filimbi tena. Na maskini huyo mama kulungu akatokea moja kwa moja kwenye uwazi huo. Sasa, ndugu, hilo si jambo la kawaida. Wasingefanya hivyo. Jambo la kwanza, asingeamka. Kama angaliamka, angalienda upande huo mwingine. Naye huyu hapa, akatokea moja kwa moja kwenye uwazi huo. Naye alijua tulikuwa pale. Na mara kinga ilipofyatuka kwenye bunduki hiyo, aligeuka na kumwangalia huyo mwindaji moja kwa moja. Badala ya kutoroka, alisimama tu pale. Masikio yake makubwa, ameyakodoa macho yake, masikio yake yamesimama juu, naye alikuwa akiangalia huku na huku.

147 Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alikuwa ni mama. Huyo alikuwa ni mtoto wake. Mtoto wake alikuwa hatarini. Maskini mwana-kondoo. . .maskini jamaa huyo alikuwa akilia, kama mtoto mchanga wa kulungu. Yeye hakuwa mnafiki. Hakuwa akijifanya. Alikuwa ni mkweli. Alizaliwa mama. Hivyo ndivyo alivyokuwa, mama.

148 Basi akalenga shabaha kwa bunduki hiyo. Nikawaza, "Unawezaje kufanya hivyo, Bert? Unawezaje?"

149 Mimi, nisingeweza kuangalia hayo. Niligeuza mgongo wangu. Nikawazia, "Bwana Mungu, mtu huyu anawezaje kuwa katili jinsi hiyo, kuulipua huo moyo mwaminifu wa mama huyo, anayemtafuta mtoto wake?" Na kumbembeleza atoke huko nje, kumdanganya na kumleta pale nje. Halafu basi, nilijua ya kwamba yeye alikuwa mwenye sha—shabaha kali, angeulipua maskini huo moyo wake mtakatifu moja kwa moja upande wake wa pili. Naye, mama, hakika angekuja maana huyo alikuwa ni mtoto wake mchanga. Hebu nena kuhusu ishara, hiyo ilikuwa ni moja yazo, ya uaminifu, kwa maana kitu fulani kilikuwa ndani. Yeye alikuwa ni mama. Ndipo nikageuza mgongo wangu. Nikasema, "Bwana Mungu, mwa—mwanadamu anawezaje kuwa katili jinsi hiyo, kufanya jambo kama hilo?"

150 Basi nikangojea na kungojea, wala ile bunduki haikutupa risasi. Niliwazia dakika yoyote ningeisikia bunduki hiyo ikilia. Nayo ilikuwa, yeye alikuwa na. . .Risasi ya punje-ya mia moja themanini, imetoa mvuke, na kuulipua moyo wake moja kwa moja kutoka kwake. Nami nikawazia, "Ni kwa nini haikufyatuka?" Nami nilikuwa nimesimama *hivi*, huku nimeyafumba macho yangu, nikiomba.

151 Na nilipokigeuza kichwa changu, kuangalia, mrututu wa bunduki ulikuwa ukienda *hivi*. Nami nikauangalia, kwa dakika chache, yeye akiufurukuta mrututu wa bunduki.

152 Akageuka na kuangalia, na hayo macho ya mjusi yalikuwa yamepata sura nyingine. Machozi yalikuwa yakitiririka mashavuni mwake. Akaitupa bunduki chini. Akasema, "Billy, yamenitosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari Zake."

153 Ilikuwa ni kitu gani? Papo hapo kwenye lundo hilo la theluji, nilimwongoza huyo mtu katili . . . Yeye ni shemasi kwenye kanisa moja sasa. Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi, kitu cha kweli, kitu ambacho hakikuwa ni theolojia fulani ama kitu cha kihistoria. Yeye alimwona Mungu katika uhalisi. Hicho ndicho kilichomleta.

154 Loo, ni wangapi humu ndani wangetaka kuwa wa aina hiyo, Mkristo zaidi, kama huyo kulungu alivyokuwa ni mama? Hakika, wakiwa na tukio halisi mbele ya mauti, ninamaanisha. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na tuinamishe vichwa vyetu.

155 Baba wa Mbinguni, wakati umechelewa. Nao watu ni wasikivu. Ni wazuri, na wanasikiliza. Na hadithi hii ndogo sasa, Bwana, ya . . . Ninaweza kukumbuka siku hiyo yenye baridi ya Novemba, nikisimama pale, na upepo kwa namna fulani ukivuma kupitia mlimani. Ninaweza kuona hayo machozi yanayolengalenga yakitiririka kwenye mashavu hayo yaliyojaa ndevu, wakati aliponishika kwa mguu. Naye akalia, na kusema, "Billy, umenena nami kuhusu Mtu ambaye ni upendo, nami—nami naona ukweli fulani hapa." Kuna kitu fulani katika kulungu huyo kilichomsukuma huko nje, Bwana, na ni umama halisi ulio mle ndani. Ilikuwa ni ishara halisi ya kwamba kulikuwako na upendo halisi na umama.

156 Ee Mungu, jalia Neno Lako linene usiku wa leo, Roho Mtakatifu halisi, wa kweli. Si kitu ambacho ni mhemko, shauku, ambacho ndivyo kilivyo, pia; bali kitu ambacho ni halisi, kwa Neno, lililodhihirishwa. "Neno, kali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo yaliyo moyoni," ambavyo uliwatambulisha manabii Wako wote. Wakati ulipokuwa duniani, Wewe uliwaita "miungu." Ulisema, "Mliwaita wale waliojiliwa na Neno la Mungu, 'miungu,' basi mwawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?"

157 Ee Mungu, ulimwengu unawajua walio wake, umekuwa kipofu miaka hii yote. Nami ninaomba, usiku wa leo, Baba, ya kwamba Wewe utayafungua macho ya watu, na utujalie usiku wa leo kuwa Wakristo halisi na waaminio halisi, kwa kuwa hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Hapa yupo aliye mkuu kuliko manabii wote. Mwana wa Mungu Mwenyewe yupo hapa, katika umbo la Roho Mtakatifu. Akiahidi, "Kidogo, bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena. Hilo neno *kosmos*, 'utaratibu wa ulimwengu,' hautaniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na, Baba, unasema Wewe "ni yeye yule jana, leo, na

hata milele," nasi tunajua ni Kweli. Loo, ninaomba, Mungu, ya kwamba utaturehemu, usiku wa leo.

158 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu. Sijui, usiku wa leo, huku tumeinamisha vichwa vyetu, kuna mtu yeyote ambaye. . . Kuwa mwaminifu kwa Mungu sasa, Uweponi Mwake. Kabla hujaona jambo lolote likitukia, bali unajua moyoni mwako ya kwamba wewe si Mkristo halisi kama vile yule kulungu alivyokuwa ni mama. Na sababu ya yeye kuwa mama ni kwa sababu alizaliwa mama. Asingeweza kujizuia kuwa hivyo. Alizaliwa mama. Na sasa kama hujazaliwa, kama huna upendo ule ule kwa ajili ya Kristo; haidhuru mtu yeyote anasema nini, unamwamini. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe ungetaka kuwa na upendo kama huo wa Kristo ndani yako, kama ule upendo wa mama uliotolewa kwa ajili yake, je, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu sasa, na kila jicho limefumbwa, waweza kuuinua mkono wako? Useme, "Niombee, Ndugu Branham," na bila shaka nitafanya hivyo. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Loo, jamani, angalieni kila mahali sakafuni, huko juu kwenye roshani, kila mahali.

159 Usione haya. Kama ukimwonea haya hapa, Yeye alisema, "Nitakuonea haya mbele ya Baba na Malaika watakatifu wakati ule." Uko katika Uwepo Wake sasa. Yeye yupo hapa. Yeye yupo hapa kabisa, yule Roho Mtakatifu mkuu. Ile Nguzo ya Moto iliyokuwa pamoja na Musa, ipo papa hapa.

160 Kumbukeni, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, alisema, "Nimetoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu." Nao wakasema, ya kwamba, "Musa aliziacha hazina za Misri, akizihesabu hazina za Kristo kuwa ni kuu kuliko shutuma zozote za Kristo, kuwa ni kuu kuliko hazina zote za Misri." Alienda nyikani pamoja na Kristo. Na msomaji yeyote wa Biblia anajua ya kwamba hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni yule Malaika wa Agano, ile Logos iliyotoka kwa Mungu, ambayo ilikuwa ni Yesu. Ndipo wakati alipokufa, alipaa juu Mbinguni. Na wakati alipokutana na Sauli, akienda zake Dameski, alikuwa tayari amegeuka akawa ile Nguzo ya Moto tena, na hata aliyapofusha macho ya Paulo kwa mng'ao.

161 Sasa Yeye yupo hapa, usiku wa leo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! ungetaka kujitambulisha mwenyewe mbele Zake, useme, "Bwana Mungu, sijapata tukio la namna hiyo. Ninataka kulipata"? Sikuombi uje hapa juu. Ninakuomba tu umwinulie mkono wako, kama ukijisikia hivyo. Kulikuwako na wengine ambao hawajainua mikono yao? Inueni mikono yenu sasa. Mungu awabariki.

162 Baba yetu wa Mbinguni, hao ni Wako. Sayansi inasema, kulingana na sayansi, hatuwezi kuinua mikono yetu. Kanuni ya uvutano huushikilia chini. Bali kuna Roho ndani ya wanaume na wanawake, nao. . . Roho mwingine aliwajia, ambaye alikuwa ni

Roho Mtakatifu, na kusema, "Inua mkono wako." Nao wakaiasi kanuni ya uvutano, na kumwinulia Mungu mikono yao, Yule aliyewaumba, "Ninataka kuwa Mkristo halisi."

163 Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamfanya kila mmoja wao Wakristo halisi, kupitia Jina la Yesu Kristo. Hao ni Wako, Bwana. Sikujua hata kidogo, siku ile wakati maskini kulungu yule alipotoka nje kondeni, ingekuwa ndiyo chanzo cha . . . Bali ilikuwa ni ishara. Lakini, Wewe unajua mambo yote, kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba utawapokea sasa. Wao ni tunu za Injili. Wao ni Wako.

164 Ulisema, "Hakuna mtu anayeweza kuwanyakua kutoka moyoni Mwangu, na kutoka mkononi Mwangu." Na, Wewe, Wewe ulisema, "Wote walio Wangu ni wa Baba Yangu. Hakuna mtu anayeweza kuwanyakua kutoka Mkononi Mwake." Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Bwana, hilo ni Neno Lako. Sasa, sio wale wanaojifanya waaminio; bali wale waaminio kweli, wana Uzima wa Milele. Wao ni Wako, Baba. Ninawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

165 Sasa iweni na kicho sana kwa muda kidogo. Sasa wakati umefika kabisa wa kufunga, bali ngojeni kidogo tu.

166 Kabla hatujafanya hivyo, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo aliahidi kuwa pamoja nasi, walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Lake? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanaoamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele? ["Amina."] Yeye, Yeye angekuwa . . . Kama alikuwa hapa, usiku wa leo, angekuwa tu kama alivyokuwa wakati huo. Angefanya jambo lile lile. Biblia ilisema, ya kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo yetu ya udhaifu." Wewe . . . Hiyo ni kweli? ["Amina."] Agano Jipya, Waebrania, mlango wa 3. "Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhai- . . . ya udhaifu wetu." Sasa iweni na imani kwa Mungu. Sasa amini tu, kweli, kwa moyo wako wote.

167 Nanyi mlio huko nje sasa, mlio huko kwenye wasikilizaji hawa, msio . . . mlio wagonjwa. Ni wangapi wenu mlio wagonjwa, inua mkono wako, useme tu, "Mimi ni mgonjwa." Sasa kwa upole kabisa, pole pole kabisa sasa, kila mtu.

168 Sasa ombeni, mseme, "Bwana Yesu, Ndugu Branham hanijui mimi, bali yale aliyosema usiku wa leo, 'Yupo hapa aliye mkuu kuliko Sulemani,' nami ninajua jambo hilo limetabiriwa kurudi. Halijakuwako duniani kwa mamia na mamia, na maelfu ya miaka. Bali Wewe uliahidi ya kwamba litarudi tena katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4, na imeahidiwa katika Luka Mtakatifu 17 na ahadi hizi zingine zote. Ulisema lingekuwa hapa

'wakati Mwana wa Adamu atakapojifunua,' kwa maana halina budi kuwa ni Neno. Maana ninii . . . "

169 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika Mwili akakaa kwetu." "Nalo Neno huyatambua mawazo." Ilikuwa ni Neno katika wale manabii. Ilikuwa ni Neno katika Mwana. Ni Neno ndani yenu, siku hii ya leo. Mnaona, Neno! Limetabiriwa, likaahidiwa. Ingawa mnapata uigaji mwingi, mashindano mengi ya kimwili, hilo haliliondoi Kwake, kutoka kwenye lile la halisi. Kuna Roho Mtakatifu halisi, Mungu halisi.

170 Sasa wewe amini kwa moyo wako wote, na uangalie huku, kwangu. Na uamini kwa moyo wako wote, useme, "Bwana Mungu, nitaomba, nami ninaomba ya kwamba—ya kwamba Wewe utamfunulia Ndugu Branham. Na unijalie niliguse vazi Lako. Nawe ugeuke, kupitia yeye, maana yeye hanijui mimi, na aniambie kwamba shida yangu ni nini. Ndipo nitajua ya kwamba Uwepo Wako upo hapa."

171 Marafiki, mnajua shida waliyo nayo Wapentekoste? Wameona mengi kupita kiasi.

172 Maskini mzee mmoja wa baharini, siku moja, alikuwa akitoka baharini, naye akakutana na mwandishi mmoja akienda baharini. Ndipo maskini mzee huyo wa baharini akamwambia yu—yule mwandishi, kasema, "Waenda wapi, mtu wangu mwema?"

173 Kasema, "Nashuka kwenda baharini. Loo, ninataka kusikia harufu ya maji yake ya chumvi. Ninataka kuona zile anga zake za bluu, mawingu meupe, na shakwe wa baharini."

174 Akasema, "Nilizaliwa humo, miaka hamsini iliyopita. Sioni kitu ambacho ni cha kuvutia kwake." Jambo ndilo hilo. Alikuwa ameiona sana, hata ikawa ni ya kawaida.

175 Hiyo ndiyo shida yetu sisi wanadamu. Tumeona mengi sana ya Mungu! Kanisa hili ambalo—ambalo limeitwa litoke katika makundi ya madhehebu katika siku za mwisho, limeona mengi sana Yake, hata limekuwa ni la kawaida sana. Mnalipuuza tu.

176 Kamwe usimwache Kristo awe wa kawaida kwako, rafiki. Kamwe usifanye hivyo. Amini tu kwa moyo wako wote na yote yaliyo ndani yako. Sasa iweni na imani kwa Mungu.

177 Sasa ombeni tu, na hebu Bwana Yesu alijalie. Sasa wewe liguse tu vazi Lake. Sijui. Wewe mguse. Anaweza kuguswa.

178 Sasa omba tu sasa. Sisemi kwamba atalifanya. Muda kidogo tu utalitatua lote. Wewe kwa—kwa—kwa namna fulani uelekeze moyo wako Kwake

179 Sasa, ni Nuru. Mtu asipige picha, picha ya kumulika. Iweni tu na kicho.

180 Sasa Hii hapa. Iko juu ya mwanamke aliyeketi hapa akiniangalia, papa hapa mwishoni, papo hapo. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, mama? Hatufahamiani. Wewe hunijui. Sikujui mimi. Lakini kama Mungu atanielezea, kama tu alivyofanya kwa yule mwanamke, akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu, ama—ama yule mwanamke aliyekuwa na waume watano; kama Bwana Yesu ata—atakupa taarifa hizo, kupitia kwangu, je! ungeamini kwa moyo wako wote? Utajua kama ni kweli ama si kweli. Vema. Ni ugonjwa wa kibofu. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako. En-he! Mnaona? Sasa, hiyo ni kweli kabisa.

181 Hapa, wewe unayeketi karibu naye. Ulikuwa ukitaka kumsaidia. Ulimgusa kwa mkono wako. Sasa ulikuwa mwema, sasa, je! unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unaamini anaweza kufanya hivyo? Shinikizo la damu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

182 Mwanamume anayeketi karibu naye, unaamini, bwana, unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Utajua kama ni kweli ama si kweli. Kuvimba kwa neva. Unaamini?

183 Maskini yule mama anayeketi pale, kidogo analia, inavyoonekana, shida yako ni wasiwasi. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa namna fulani umetiwa uvuli, wewe hudhoofika mchana, unafikiri unaingia kichaa. Ibilisi hujaribu kukwambia hivyo. Lakini, huingii. Yote yamekwisha, tangu usiku wa leo, sasa. Unaona? Umepata ushindi. Umekuacha. Huo uvuli mweusi, uliokuwa juu yako, umekuacha.

184 Ulikuwa ukilia pale, wewe unayeketi karibu naye, mama. Hilo, hilo lilikusisimua sana. Sasa je! unaamini kwamba mimi ni nabii Wake, ama mtumishi Wake? Hiyo huwakwaza watu wengine, mnaona. Kwa hiyo, wewe, sikujui mimi. Hatufahamiani. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Vema. Una ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa figo, na una upungufu wa damu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

185 Maskini mama huyu anayeketi hapa, kidogo ni mnene, amevaa nguo nyekundu yenye mistari myeusi. Anaomba. Anataka aitwe katika mstari huu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Je! unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Rafiki yako atapona. Hiyo shida ya kiroho itakwisha. Na ugonjwa wako wa kike utakuacha, kama utamwamini Mungu kwa moyo wako wote. Sasa, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kama hilo ndilo ulilokuwa ukiombea, inua mkono wako kusudi watu waweze kuona yale unayofanya. Unaona? Vema.

186 Iweni tu na imani kwa Mungu. Mtu fulani huko nyuma... Sio lazima uwe umeketi hapa mbele. Huko nyuma kabisa; amini kwa moyo wako wote.

187 Huko nyuma kabisa, yupo mwanamke. Ana uvimbe ubavuni mwake. Anaomba. Ataukosa.

Bwana Mungu, nisaidie, naomba.

188 Bibi Goodman, unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu atauondosha uvimbe huo kutoka ubavuni mwako? Vema. Sogea, inua mkono wako juu kabisa, kusudi watu waweze kukuona. Hatufahamiani kabisa, sijapata kumwona. Huyo hapo. Je! mambo hayo ni kweli? Inua mkono wako. Vema.

189 Mama anayeketi pale, pale karibu na mwisho, ana ugonjwa wa kibofu nyongo. Naye, pia, ana kisukari, ugonjwa wa moyo. Bibi Holderfield, amini kwa moyo wako wote, mama, nawe unaweza kuponywa hapo sasa.

190 Naomba msisogee-sogee, enyi watu. Na—nawaomba, katika Jina la Kristo, msifanye hivyo. Mnaona, magonjwa hutoka kwa mmoja yakaingia kwa mwingine. Mnaona? Kutokuamini ndicho kitu kibaya sana kilichopo ulimwenguni. Iweni tu na imani.

191 Huyu hapa maskini mama anayeketi hapa, akimwombea mumewe. Yeye hunywa pombe. Hiyo ni kweli. Unaomba ya kwamba ataacha kunywa. Hiyo si ni kweli? Vema. Sikujui mimi. Je! una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji moja; ni imani tu uliyo nayo. Uligusa kitu Fulani. Uko futi ishirini ama thelathini kutoka kwangu. Ulimgusa Kuhani Mkuu.

192 Maskini mwanamke yule pale nyuma anamwombea mumewe, pia, anayeketi nyuma yake. Hiyo ni kweli. Mume wako ni mtu mwenye wasiwasi, kitu kama wasiwasi wa akili. Yeye haonekani wakati huu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Nawe una kasoro mkononi mwako. Una mzio, kitu kama hicho. Na ukishika kitu, kinaufanya mkono wako kuharibika. Hiyo si ni kweli? Bibi Patty ndilo jina lako. Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Amina. Unaona? Nimekuomba uniamini.

193 Vipi kuhusu mama huyu anayeketi hapa? Una alama usoni mwako, kama kansa ndogo ya ngozi. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Unaamini? Sikujui. Wewe ni mgeni kwangu. Hicho sicho unachoombea hasa. Unaombea ugonjwa wa moyo ulio nao. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Mama huyu anayeketi hapa. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuupokea uponyaji wako. Mumeo alipata wake jana usiku, mbona usiupate? Mwanamke aliyekuwa mhubiri. Sasa amini kwa moyo wako wote, nawe. . . Sasa, unaona, ili kwamba tu upate kujua. Kwa namna fulani ulikuwa ukiswali niani mwako, unaona. Sasa umeridhika, sivyo, kwamba Yeye hufanya hivyo? Vema. Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Mwamini Mungu.

194 Unawazia nini juu ya kisukari hicho, bwana, uliyeketi hapa huku umeinua mkono wako? Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukiponya kisukari na kukupa afya? Unaamini? Vema, bwana, Mungu anaweza kukuponya.

195 Wewe ni mgeni kwangu, pia. Kama utaamini kwa moyo wako wote! Yupo mtu anayeketi pale, aliye na ugonjwa wa moyo, ana shida fulani mgongoni mwake. Bw. Easter. Alijeruhiwa kwenye ajali ya garimoshi, iliyosababisha jambo hilo. Kama hiyo ni kweli, simama, Yesu Kristo atakuponya na kukupa afya.

196 Ni wangapi wenu wanaoamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Mnaamini hilo? ["Amina."] Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, alipitia kote jengoni upesi. Mnaamini sasa ya kwamba Yeye yupo hapa? ["Amina."] Yeye yupo papa hapa sasa. Hilo ni hakika. Hivyo ndivyo alivyosema ingetukia hasa, "Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya; zaidi ya haya mtayafanya, kwa maana Mimi naenda kwa Baba Yangu." Wakati mmoja mwanamke alimgusa, Yeye akawa dhaifu sana, akasema, "Nguvu zimenitoka," Naye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Mimi ni mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa neema Yake. "Zaidi ya hizi mtazifanya." Ninajua tafsiri ya Mfalme James inasema, "kubwa zaidi." Lakini katika ile ya asili, inasema, "*Zaidi* ya hizi mtazifanya, kwa maana Mimi ninaenda kwa Baba Yangu."

197 Sasa mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini Uwepo Wake upo hapa? ["Amina."] Basi kwa nini msiwekeane mikono, ninyi waaminio, na umwombee mwenzako anayeketi karibu nawe. Kila mmoja wenu wekeaneni mikono, na uamini kwa moyo wako wote sasa unapoomba. Ombeni jinsi mnavyoomba kanisani. Aminini jinsi mmeamini daima. Sasa hebu Roho huyo wa Mungu, aliyekufanya Mkristo, awe mkuu tu na wa kifalme kwako unapomwombea mtu huyo, ili kwamba kama vile yule mama kulungu alivyokuwa na umama ndani yake, ile Roho aminifu ya Kristo iliyoko hapa sasa.

198 Hilo, ulimwengu hauamini. Ulimwengu unalichukia. Ulimwengu haulielewi. Biblia ilisema usingelielewa. Ulimwengu unawajua walio wake.

199 Naye Mungu anawajua walio Wake. Mungu aliliahidi. Ni Kweli. Kwa hiyo na anisaidie, ni Kweli! "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

Tuombeni sasa.

200 Bwana Yesu, hizi hapa baadhi ya leso zimewekwa hapa, ambazo ni za wagonjwa na wanaoteseka, nami ninaweka mikono yangu juu yake. Kwa sababu, tunafundishwa katika Biblia ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo leso na nguo, nao pepo wachafu wakawatoka watu, nao wakaponywa magonjwa. Sasa sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Yesu. Nami ninaomba ya kwamba utazienzi hizi, kwa ajili ya watu hawa ambao wasingeweza kuwa mkutanoni.

201 Jalia, wakati zikiwekwa juu ya watu, jalia itukie, kama vile mmoja wa wale waandishi alivyosema wakati—wakati Bahari ya Shamu ilipokuja mbele ya wana wa Israeli, "Mungu alichungulia

chini kupitia kwenye hiyo Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira, ndipo bahari ikaogopa kwa sababu ilikuwa imesimama njiani mwa jukumu lao, hao waaminio, nayo bahari ikarudi nyuma na—na hao waaminio wakavuka wakaingia kwenye nchi ya ahadi."

202 Bwana Mungu, angalia chini kupitia Damu ya Mwanao, Yesu Kristo, usiku wa leo, juu ya leso hizi, juu ya wasikilizaji hawa hapa, waliowekeana mikono, wakiombeana. Wewe ulisema, "Ungameni makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Kwa maana, maombi ya mwenye haki yana nguvu tena yafaa sana, akiomba kwa bidii."

203 Ninaomba, Mungu, wakati M—Mkristo aliyetubu usiku wa leo anapomwombea mtu aliyemwekea mikono, jalia Nguvu za Roho Mtakatifu zije juu ya mtu huyo. Jalia Roho awahuishie, Bwana, ule uhalisi. Jalia wasiukose, Bwana. Jalia wasiwe kama kitu kitakachoukosa, Baba. Jalia Birmingham ipate ono lake sasa, la Uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka, aliye mkuu kuliko manabii wote, aliye mkuu kuliko wahubiri wote, aliye mkuu kuliko mapapa wote ama watawala, ama wowote wale. Ni Yesu Kristo, "yeye yule jana, leo, na hata milele," akijithibitisha Mwenyewe katika siku za mwisho, kwa Neno Lake lililoahidiwa. Tujalie, Bwana. Ninaomba imani hii, ombi hili la imani, kwa ajili yao, wanapoombeana. Katika Jina la Yesu Kristo, tunawakabidhi Kwako.

204 Sasa kila mmoja wenu, huku mkono wako ukiwa juu ya mtu fulani, sasa fungeni tu macho yenu, na mkumbuke: yule Kristo aliyeahidi jambo hili, amekuja hapa na kujithibitisha Mwenyewe.

205 Naam, nimemwona mtu akiponywa pale pale, mwenye TB, anayeketi papa hapa nyuma mbele yangu. Sasa kama mkininii tu. . . Inaendelea tu kila mahali, kila mahali jengoni. Hakika kama Mungu. . .

206 Mwanadamu anaweza kusema lolote; hilo halilifanyi kuwa kweli. Bali wakati Mungu anaposhuka na kulisema, na kulithibitisha na kulihakikisha kwamba ni Kweli; kutokuliamini, ni dhambi isiyosameheka. Yesu alisema, "Haitasamehewa, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao."

207 Maandiko yanaahidi hili, na hapa limethibitishwa moja kwa moja mbele zenu. Enyi watu, katika Jina la Yesu Kristo, mpokeeni wakati Yeye—wakati Yeye akiwa hapa mbele zetu usiku wa leo, tunapokuwa pamoja Naye. Je! mtaamini?

208 Na wote wanaomwamini kweli na kumkubali kama Mwokozi wenu, ama kama mponyaji wenu, mwaweza kusimama kwa miguu yenu mkatoe ushuhuda, "Nitasimama kama ushuhuda. Ninaamini kweli, na sasa ninaukubali uponyaji

wangu, wokovu wangu. Na haja zangu zote, katika Uwepo wa Kristo, sasa nakubali."

209 Jamani, angalieni kote jengoni, karibu kusanyiko lote limesimama. Ajabu! Hilo ni zuri. Sasa yote yamekwisha, kama utaamini. "Kama unaweza kuamini!"

210 Sasa hebu na tufunge macho yetu na kuinua mikono yetu, na kuimba, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Na tumpe sifa tunapoimba sasa, tumwimbie sifa hizi.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

211 Na tuinue mikono yetu, na kusema, "Bwana asifiwe!" [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe!"—Mh.] Bwana asifiwe! ["Bwana asifiwe!"] Bwana asifiwe! ["Bwana asifiwe!"]

> Nampenda, (kila mtu) nampenda,
> Kwani . . .

212 Nafikiri ya kwamba wewe utawaruhusu waondoke, Ndugu Urshan. [Mtu fulani anasema, "Vipi kuhusu wale waliotaka kuokoka?"] Nitawaomba waje mbele.

> Na kununua wokovu wangu
> Kalvari . . .

213 Sasa inamisha kichwa chako kwa muda kidogo tu. Piano, mpiga kinanda na mpiga piano waendelee moja kwa moja.

214 Sijui, usiku wa leo, imani yako ingali inaamini. Sijui kama unaamini ya kwamba Mungu anayeweza kuniambia siri za moyo, kuthibitisha ya kwamba . . .Haimbidi kufanya hivyo, sasa, bali Yeye alisema angelifanya. Wakati Yesu alipokuja kwa mara ya kwanza, haikumbidi kuponya, bali alisema ataponya. "Naye alifanya hivyo yapate kutimizwa yale yaliyonenwa na nabii." Naye anayafanya usiku wa leo kwa sababu manabii walisema angeyafanya, Naye Yesu alisema angeyafanya, pia.

215 Sasa sijui kama wewe, unayeutaka ule upendo wa Mungu moyoni mwako kama—kama yule mama kulungu alivyompenda mtoto wake mchanga, unautaka upendo huo moyoni mwako kwa ajili ya Kristo, nawe unaamini angeyasikia maombi yetu, naomba uje usimame hapa wakati tukikuombea. Tunapouimba huo mara nyingine tena, njoni tu papa hapa juu. Mnakiri hadharani basi, njoni tu moja kwa moja na msimame hapa. Kama mnaamini, maombi, maombi yangu yatawasaidia, pandeni papa hapa juu tunapouimba huu tena.

216 "Na . . ." Sasa thibitisha unampenda, kwa kuja. ". . . Yeye, na . . ." Mungu akubariki.

> Kwani alinipenda kwanza

217 Na mteremke kutoka kwenye roshani, nasi tutawangojea. Hilo ni sawa. " . . . wangu . . . " Kama kweli wewe ni mkweli, njoo huku sasa.

> . . . wokovu
> Mtini Kalvari.

218 "Na . . . " Watu wanatoka kwenye roshani, wanashuka. Kila mtu na aimbe sasa. "Na . . . " Ingieni moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa, popote pale, njoni moja kwa moja.

> Kwani alipenda kwanza . . .

219 Kumbukeni, Mungu yule atakayekutana nawe kwenye ile Hukumu, amekutana nawe hapa kanisani usiku wa leo.

> . . . wokovu wangu
> Mtini Kalvari . . .

220 Sijui kama wahudumu wote hapa, walio na shauku ya nafsi zilizopotea, ambao wangali wana ono la watu wahitaji, kama mtakuja huku sasa miongoni mwa watu; ninyi wahudumu wote humu ndani, kila mhudumu anayeamini ya kwamba Mungu angali atamwokoa mwenye dhambi. Huenda ukaona moja ya mambo yaliyo makuu sana likitukia sasa hivi, uliyopata kuona. Hili ndilo Roho Mtakatifu analopenda.

> Nampenda . . .

221 Sasa thibitisha jambo hilo. Thibitisha kwamba una shauku, unampenda. Kama unawapenda walio Wake, Yeye, unawapenda watoto Wake.

> . . . mpenda
> Kwani . . .

222 Sasa jipenyezeni miongoni mwa watu hawa hapa! " . . . penda . . . " Njoni moja kwa moja huku juu na mwingie kati ya watu hawa, moja kwa moja namna hii, na mjipenyeze ndani kabisa na kuwawekea mikono. Na mje moja kwa moja huku juu sasa, tunaenda kuomba. Ninaamini Roho Mtakatifu atamwagwa juu ya watu, usiku wa leo, papa hapa kwenye kusanyiko.

> . . . mtini Kalvari.
> Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,

Mnapendana Naye; mnaweza kulisoma Neno Lake.

> Na jinsi ninavyompenda Yesu,
> Loo, jinsi . . .

223 Sasa ufungie mbali ulimwengu kutoka kwako sasa. Ufungie ulimwengu wote mbali na wewe. Unaona?

> Kwani alinipenda kwanza.
> Loo, jinsi nina- . . . (vizuri sana)
> Loo, jinsi . . .

224 Sasa, wahudumu, mchukue mtu fulani katika ninii yako... Niweke sasa. Wahudumu ingieni ndani, ingieni moja kwa moja katikati ya watu.

> Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
> Kwani alinipenda kwanza...

225 Sasa yeye amesimama hapa. Anajua kila kitu kilicho moyoni mwako. Si mnaamini anajua hayo? Papa hapa, haikuwa ni siri. Anajua yale unayonena, yale unayomaanisha.

226 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kila mmoja, kote kwenye wasikilizaji, ninyi ambao hata msingeweza kufika hapa. Sasa hebu tuombe.

227 Kila mmoja wenu na aungame tu makosa yako yote, ungama kutokuamini kwako kote. Useme, "Bwana Yesu, labda nilikuwa mfuasi wa kanisa, wakati mmoja. Nilienda kanisani, bali kamwe sikuridhika. Kulikuwa na kitu fulani...Loo, huenda nilininii, huenda nilipaza sauti. Huenda nilinena kwa lugha. Mimi, huenda nilijiunga na kanisa." Mambo hayo yote, ni mazuri. Sina kitu dhidi ya jambo hilo, bali hilo silo ninalonena habari zake.

228 Ninazungumza kuhusu upendo wa Mungu ambao kweli uko kule chini. Huo ni Roho Mtakatifu. Huo ndio. Na unahitaji huo, kitu ambacho kimekolea kweli, ambacho kitalifanya Neno la Mungu liishi kupitia kwako na kutenda kupitia kwako. Unaona, hamna mashina ya uchungu katika mkondo huo, Roho Mtakatifu anatiririka tu moja kwa moja kupitia kwako. Hilo ndilo unalohitaji.

229 Sasa inamisha tu kichwa chako na uombe kwa uchaji. Nanyi wahudumu wawekeeni mikono yenu sasa.

230 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe, usiku wa leo, kusanyiko hili la watu wanaosimama hapa wakitubu, wakijua ya kwamba wamekuwa makosani. Huenda ikawa, labda, nia na malengo, pia, yamekuwa ni mabaya. Lakini, usiku wa leo, wamekuja, wakiamini, wakiamini ya kwamba Wewe utasamehe kila dhambi. Wengi wao wameenda kanisani, kwa miaka mingi. Wengi wao wame—wamefanya mambo mengi ya misaada. Lakini, Bwana, usiku wa leo wanataka uhalisi, wanataka ule utamu, kile—kile kitu walichopungukiwa nacho maishani mwao, yule Roho Mtakatifu wa Mungu anayetenda kazi mle ndani, mfano wa Neno.

231 Nao watumishi Wako, wahudumu, watumishi Wako, wamewawekea mikono yao. Nasi tunawaombea, maombi haya, na kuomba, Bwana, ya kwamba huu utakuwa ndio ule wakati ambapo hakuna njia nyingine ila moja kwa moja moyoni mwao, itakuwa siku moja, milele, katika Uwepo Wako, litatuliwe sasa hivi. Jalia Roho Mtakatifu aingie maishani mwao sasa hivi na kuwafanya watamu, Bwana, kwa—kwa ile Asali kuu ya Mbinguni. Na uwape tukio ambalo litakuwa ni tukio la milele, kusudi ule Uwepo mkuu wa Mungu aliye hai uje kwa ujasiri

maishani mwao na kuwapa kile wanachohitaji sasa hivi. Tujalie, Mungu wa Milele. Wao ni Wako. Ninawakabidhi Kwako, kama tunu za upendo, na kama dhabihu kama zile wanazotoa hapa. Pia jalia Roho Mtakatifu alifanye tu halisi kwao sasa. Mungu, tujalie, katika Jina la Yesu.

232 Mchungaji wenu ataomba. [Huyo ndugu anaomba—Mh.] Naam, Bwana. Naam, Bwana. Tujalie.

Ishara Za Kimaandiko Za Wakati Huu SWA64-0410
(Scriptural Signs Of The Time)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 10 Aprili, 1964, katika National Guard Armory huko Birmingham, Alabama, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org